# TASWIRA DUMIFU ZA UANA KATIKA FASIHI YA KISWAHILI YA WATOTO

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION
FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

NA

ENOCK SEME MATUNDURA

*2007*

***Tasnifu iliyotolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Master of Arts katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi.***

University of NAIROBI Library
0442022 0

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa minajili ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

..........................................................................................

ENOCK SEME MATUNDURA

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama washauri na wasimamizi tulioteuliwa na chuo.

..........................................................................................

DKT RAYYA TIMAMMY

**(Msimamizi)**

..........................................................................................

DKT ZAJA OMBOGA

**(Msimamizi)**

## *TABARUKU*

Tasnifu hii namtabarukia Amu yangu:

***John Mamboleo Onsando***

Aliyeaga dunia nilipokuwa ninaiandika

# YALIYOMO

Mada ........................................ i

Ikirari ........................................ ii

Tabaruku ........................................ iii

Yaliyomo ........................................ iv

Shukrani ........................................ ix

Ikisiri ........................................ xi

Orodha ya Vifupisho ........................................ xiii

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Utafiti ........................................ 1

1.1 Somo la Utafiti ........................................ 5

1.2 Madhumuni ya Utafiti ........................................ 5

1.3 Nadharia Tete ........................................ 6

1.4 Sababu za Kuchagua Somo Hili ........................................ 7

1.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ........................................ 8

1.5.1 Maandishi Kuhusu Maswala ya Uana ........................................ 8

1.5.2 Maandishi Kuhusu Fasihi ya Watoto ........................................ 16

1.6 Upeo na Mipaka ........................................ 18

1.7 Njia za Utafiti ........................................ 20

1.8 Msingi wa Kinadharia ........................................ 21

1.8.1 Mkabala wa Uana ........................................ 23

1.8.2 Ufeministi ........................................ 25

1.8.2.1 Uibukaji na Maendeleo ya Kihistoria ........................................ 25

1.8.2.2 Ufeministi wa Kiharakati ........................................ 30

1.8.2.3 Chukulizi za Kimsingi za Ufeministi ........................................ 31

1.8.2.4 Njia za Utekelezwaji ........................................ 33

Tanbihi ........................................ 34

## SURA YA PILI

### FASIHI YA WATOTO NA MAJUKUMU YAKE, UANA, JINSIA NA TASWIRA DUMIFU

2.1 Utangulizi ........................................ 36

2.2 Fasihi ya Watoto na Sifa Zake ........................................ 36

2.3 Majukumu ya Fasihi ya Watoto ........................................ 38

2.4 Fasiri ya Dhana 'Uana' na 'Jinsia' ........................................ 40

2.5 Swala la Uana Katika Mtazamo wa Kihistoria ........................................ 41

2.6 Uana na Ugavi wa Majukumu ........................................ 43

2.7 Uana na Elimu ........................................ 43

2.8 Taswira Dumifu za Uana na Jinsi Zinavyobainishwa ........................................ 43

2.9 Hitimisho ........................................ 47

Tanbihi ........................................ 49

## SURA YA TATU

## TASWIRA DUMIFU ZA UANA KATIKA *MSICHANA MLEMAVU NA NDUGU ZAKE*, *MWANASESERE WA MOSI* NA *MGOMBA CHANGARAWENI*


3.1 Utangulizi ..........50

3.2.0 *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* ..........51

3.2.1 Muhtasari wa *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* ..........51

3.2.2 Taswira Dumifu za Uana Katika *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* ..54

3.2.3 Wahusika, Hulka na Majukumu yao ..........56

3.2.3.1 Wahusika na Hulka Zao ..........56

3.2.3.2 Majukumu ya Wahusika ..........59

3.2.3.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume ..........61

3.3.0 *Mwanasesere wa Mosi* ..........61

3.3.1 Muhtasari wa *Mwanasesere wa Mosi* ..........61

3.3.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Mwanasesere wa Mosi* ..........62

3.3.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume ..........66

3.4.0 *Mgomba Changaraweni* ..........67

3.4.1 Muhtasari wa *Mgomba Changaraweni* ..........67

3.4.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Mgomba Changaraweni* ..........68

3.4.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume ..........71

3.5 Hitimisho ..........72

Tanbihi ..........74

## SURA YA NNE

### TASWIRA DUMIFU ZA UANA KATIKA *NDOTO YA RIZIKI*, *SIKU YA WAJINGA* NA *ALITOROKA KWAO*


4.1 Utangulizi ......75

4.2.0 *Ndoto ya Riziki* ......76

4.2.1 Muhtasari wa *Ndoto ya Riziki* ......76

4.2.2 Taswira Dumifu za Uana Katika *Ndoto ya Riziki* ......77

4.2.3 Majukumu ya Wahusika ......80

4.2.4 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume ......82

4.3.0 *Siku ya Wajinga* ......82

4.3.1 Muhtasari wa *Siku ya Wajinga* ......82

4.3.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Siku ya Wajinga* ......85

4.3.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume ......90

4.3.0 *Alitoroka Kwao* ......90

4.4.1 Muhtasari wa *Alitoroka Kwao* ......90

4.4.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Alitoroka Kwao* ......92

4.4.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume ......94

5.0 Hitimisho ......95

Tanbihi ......96

## SURA YA TANO

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi ........................................................................................97

5.2 Muhtasari wa Matokeo ..........................................................................97

5.3 Kuhusu Nadharia Tete ..........................................................................100

5.4 Matatizo ...............................................................................................101

5.5 Mapendekezo .......................................................................................101

# SHUKRANI

Kazi ya utafiti huwa si ya mtu mmoja; ni ya kikoa. Hivyo basi ningependa kutoa shukrani za dhati kwa watu mbalimbali waliofanikisha juhudi hizi. Mosi, nawashukuru ghaya wasimamizi wangu, Dkt Rayya Timammy na Dkt Omboga Zaja ambao waliufuatilia utafiti huu kwa makini hatua baada ya hatua na kunielekeza na kunikwamua nilikokuwa nimekwama. Mbali na hayo, walikuwa tayari kunitengea muda wao adimu kunikosoa nilikokuwa nimekwenda kombo. Ninaamini kwamba katika kunishauri, hawakumasikinika kitaaluma bali walitajirika zaidi.

Pili, ninawashukuru wahadhiri wangu wote katika Idara ya Isimu na Lugha kwa kuwa dira maridhawa katika bahari ya elimu yenye matatizo mengi ambayo wakati mwingine ni ya kukatisha tamaa. Hawa ni pamoja na Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz, Profesa Lucia Ndonga Omondi, Profesa Kithaka wa Mberia, Dkt Andrew Mwenda Mbatiah (Mwenyekiti, Idara ya Isimu na Lugha), Dkt John Hamu Habwe, Dkt Kineene wa Mutiso, Dkt Murage Evans Mbuthia, Dkt Kyallo Wadi Wamitila na Dkt Tom Mboya Olali. Wengine ni Bw Basilio Gichobi Mungania na Bw Hezron Matagaro Mogambi. Siwezi kusahau mchango wa Dkt Mbatiah, Dkt Wamitila, Dkt Habwe na Mwalimu Mogambi ambao waligundua kipawa changu cha uandishi bunifu na kukikuza kimaksudi.

Kadhalika, namshukuru Profesa Kimani wa Njogu (IFRA) ambaye alinipa ushauri katika hatua za awali za utafiti huu. Aidha, Profesa Njogu amekuwa katika msitari wa mbele kunikuza kitaaluma bila yeye kujua. Nawashukuru pia Profesa Inyani Kenneth Simala (Chuo Kikuu cha Maseno), Ndugu John Kobia Mwithalii wa Chuo Kikuu cha Masinde Muliro na Ndugu Ng'ang'a Samuel Irungu kwa kunihimiza kila mara kujitahidi katika kila nilifanyalo.

Nawashukuru pia wakutubi wa Chuo Kikuu cha Nairobi na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Aidha, natoa shukrani maalum kwa kaka yangu, Dkt James Micah Onsando na mkewe, Bi Margaret Onsando kwa kunilea tangu nilipokuwa mdogo na kunipa mazingira mazuri ya kusoma, kando na kufuatilia kwa makini hatua zangu katika elimu. Fauka ya hayo

walitoa mchango aali katika kunilipia karo ili kuhakikisha kwamba ninakamilisha masomo haya kwa wakati unaofaa.

Ningependa pia kuwashukuru wazazi wangu, baba yangu Mzee Micah Matundura Onsando, Mama Miriam Nyangweso na Mama Rebecca Mokeira ambao wametulea na kutufunza kunyenyekea na kuwaheshimu binadamu wa hadhi na tabaka zote. Aidha, nawashukuru ndugu na dada zangu: Gideon Lumumba, Ken Nyabuto, Druscillah Nyasuguta, Jane Kwamboka, Ochego Matundura (ambaye sasa ni marehemu), Pamella Kwamboka, Peris Makiya, Matino Matundura (ambaye sasa ni marehemu) Joan Nyaboke, Dellilah Moraa, Priscillah Kerubo na Norah Nyansarora kwa kunihimiza kila mara nisome hadi ukomo wa elimu na kuamini kwamba 'nikifaidi mimi tumefaidi sote'.

Vilevile namshukuru mwajiri wangu, Shirika la Habari la Kenya (KBC) kwa kuniruhusu kuendelea na masomo hasa kwa kuandaa ratiba ya kazi iliyoniruhusu kuhudhuria masomo bila kutatiza shughuli zangu kikazi.Namshukuru kwa dhadi Mhariri Mkuu, Hiram Mucheke na wafanyakazi wote katika kitengo cha Uhariri na Ufasiri wa Habari. Ningependa kuwataja baadhi kwa majina: Ndugu Ngulamu Mwaviro (Mkuu wa Kitengo cha Ufasiri), Edward Kadilo, Rose Kamau, Aggrey Muteve, Jonna Ngare na Ndugu Henry Okello. Kwenu nyote, shukrani jazila.

Siwezi kamwe kuwasahau wazamili wenzangu, Ogoro Evans Makori, Ontiri Samson Ongarora, Gakuo Henry Njoroge, Mutua John Musyoka, Kioni Gabriel Mburu na Mogere Gerald Okioma kwa mijadala mingi tuliyokuwa nayo na kukimiana kwa hali na mali. Ninaamini kwamba ushirikiano huo ulituwezesha kutambua kwamba 'kutojua kwamba hujui ndio mwanzo wa kuelimika'.

Mwisho, na muhimu sana, namshukuru mke wangu mpenzi, Lilian Mokeira Arama na mwanangu, Ernest Griffin Matundura (Jnr) kwa kuvumilia hali ya upweke nilipokuwa ninazama na kuibuka katika bahari ya masomo yenye misukosuko mingi.

# IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu limekuwa ni kubainisha jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Nadharia tete tatu zilizoongoza utafiti huu ni: Mosi, taswira dumifu za uana zinadhihirika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Pili, wahusika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto husawiriwa kwa njia sawa bila kubaguliwa kwa misingi ya jinsia zao. Mwisho, waandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili ya watoto huwakilisha idadi sawa ya wahusika wa kike na kiume katika kazi hizo. Kupitia kwa utafiti huu, nadharia tete ya kwanza imethibitishwa kuwa kweli. Lakini nadharia tete ya pili na ya tatu zimethibitishwa kuwa si kweli. Mikabala ya uana na ufeministi ambayo imetumika katika utafiti huu ilitoa msingi madhubuti katika utafiti huu ila tulilazimika kuitumia kwa tahadhari kwa sababu inaakisi mno tamaduni za Kimagharibi. Kuna juhudi zinazofanywa za kutafuta mkabala wa ufeministi unaoafiki zaidi uhakiki wa fasihi ya Kiafrika.

Tasnifu hii ina sura tano zinazoshughulikia kipengele cha taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto ifuatavyo:

Sura ya kwanza inatoa kwa ujumla mwelekeo wa kuchunguza jinsi taswira dumifu za uana zinavyoweza kudhihirishwa katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Inahusisha sehemu kuhusu somo la utafiti, malengo, nadharia tete, sababu za kuchagua somo hili, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa kinadharia, upeo na mipaka na njia za utafiti.

Sura ya pili imejadili kwa ujumla kuhusu fasihi ya watoto, sifa na majukumu yake, tofauti kati ya dhana 'uana' na jinsia. Aidha sura hii imezungumzia taswira dumifu.

Katika sura za tatu na nne, tumechunguza matini za tungo za fasihi ya Kiswahili ya watoto za waandishi wa kiume (androtexts) na kike (gynotexts) mtawalia ili kubainisha jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza. Kadhalika katika sura hizi, tumechunguza iwapo wahusika wa kike na kiume wamewakilishwa kwa idadi sawa kwenye matini hizo.

Sura ya tano ni hitimisho. Ina sehemu za muhtasari wa matokeo ya utafiti huu kwa misingi ya nadharia tete zilizoongoza uchunguzi huu, matatizo tuliyokumbana nayo katika utafiti huu na mapendekezo kuhusu utafiti zaidi.

## VIFUPISHO AMBAVYO VIMETUMIKA KATIKA UTAFITI HUU

Uk. - Ukurasa

Taz. - Tazama

Khj. - Kama hapo juu

Rej. - Rejelea

n.k. - Na kadhalika

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Usuli wa Utafiti

Maswala ya kiuana ni ya kimsingi sana katika jamii yoyote na yametawala fasihi ya Kiswahili kwa hadhira pevu na fasihi ya Kiswahili ya watoto. Utoto ni awamu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Maoni ya Fox (1993) kwamba, kila tukisomacho hutujenga na kutufanya tuwe tulivyo katika uwasilishaji wa taswira yetu kama wasichana na wanawake na kama wavulana na wanaume yanafumbata umuhimu wa awamu hiyo. Wataalamu wa maswala ya saikolojia ya watoto wameonyesha kwamba ukongomelevu wa tabia za mtu mzima zina chanzo chake utotoni. Tunaamini kwamba ubwiaji wa taswira dumifu za uana kutokana na fasihi ya watoto ya Kiswahili unaweza kuchangia hali hii na hivyo basi pana haja ya waandishi wa fasihi hiyo kudhibiti taswira hizo. Wahakiki waliotangulia katika uwanja huu hawajaitilia maanani fasihi ya Kiswahili ya watoto. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hili.

Vitabu vyote vya kiada na vile vya fasihi vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi aghalabu huwa na hadithi kuhusu watu, namna wanavyohusiana baina yao na mazingira wanamoishi (Kabira na wenzie, 1995). Fasihi husheheni maarifa ya kiakademia na maarifa kuhusu ulimwengu kwa jumla wa jamii husika. Katika kufanikisha uvushaji huu wa maarifa hadi kwa wasomaji, waandishi wa fasihi hubuni ulimwengu ambao wasomaji wanaweza kuutambua kwa urahisi na kujinasibisha nao. Hali hii hurahisisha uvushaji wa maarifa. Kwa hivyo, waandishi huuisha matini kwa

kuelezea hadithi kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja jinsi watu huhusiana na kukimiana maishani.

Fasihi ya watoto ni nyenzo ya kuimarisha mtagusano wa kijamii mbali na uvushaji wa maarifa ya kiakademia. Kwa kuwa ulimwengu unaosawiriwa katika fasihi ni ulimwengu wanamoishi wanawake na wanaume, wavulana na wasichana, fasihi ya watoto huonyesha ulimwengu wa kiuana miongoni mwa jamii ambazo huegemea kigezo hiki katika utambulishaji wa watu wa jinsia tofauti na majukumu yao. Hii ina maana kwamba fasihi hiyo hutoa hadithi kuhusu wanawake na wasichana na wanaume na wavulana ambazo zinaweza kubainishwa kwa kuchunguza matini ya hadithi hizo.

Usomaji wa fasihi na hasa fasihi ya watoto unaweza kuwaathiri watoto ama kwa njia ya moja kwa moja au njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Kwa mfano, iwapo kwenye matini wasichana wanaonyeshwa kuwa kila mara wao ndio wanaowasaidia wazazi nyumbani huku wavulana wakiwekwa pembezoni, kuna uwezekano kwamba hadhira ya watoto wanaoisoma matini hiyo wataibwia hali hiyo kuwa kiwakilishi cha uhalisia katika jamii. Uchunguzi umebainisha kwamba watoto hubwia kwa haraka taswira dumifu za tamaduni, hasa kuhusu majukumu ya kijamii yanayopaswa kutekelezwa na wamaume na wanawake (Fisher - Thompson, 1993; O'Keefe & Hyde, 1983, Signorella, Bigler, & Liben, 1993; Turner, Gervai & Hinde, 1993). Ingawa uchunguzi huu ulifanywa katika tamaduni za Kimagharibi ambapo uana ni utaratibu wa kuipanga jamii, unaakisi kwa kiasi fulani hali hiyo katika tamaduni za Kiafrika ambazo pia zimeathiriwa na tamaduni hizo.

Jinsi suala la uana linavyoshughulikiwa katika fasihi ya watoto huchangia pakubwa taswira dumifu inayokuzwa na kukitwa miongoni mwa watoto hao na majukumu yao ya kiuana katika jamii. Fasihi hii husomwa katika kipindi ambacho watoto wanakua na kuamini mambo mengi wanayoyasoma kuwa ndio uhalisia wa maisha. Katika kipindi hicho watoto hawana uwezo wa kuchuja yepi ya kubwia na yepi ya kutupiliwa mbali. Kwa hivyo, baadhi ya taswira dumifu za uana wanazokumbana nazo katika fasihi hukongomelewa katika maisha yao na kuwaathiri wanapokuwa watu wazima.

Taswira dumifu ni maoni ya kijumla na mitazamo inayoshikiliwa na jamii husika kuhusu kundi fulani la watu. Maoni na mitazamo hiyo aghalabu huwa hasi na inaweza kutumiwa kuhalalisha ubaguzi fulani. Wakati mwingine taswira dumifu zinaweza kuakisi maarifa na uhalisia wa kijamii. Taswira dumifu hutokana na mikakati ya kutilia chumvi, ujumlishaji, kuwasilisha mawazo ya kijamii kwa kuyafanya yaonekane ya kiasilia, ubaguzi wa rangi, jinsia, miongoni mwa mikabala mingine (Allport, 1954).

Taswira dumifu zinaweza kudhihirika katika makundi mbalimbali kwa misingi ya umri, kabila, uana, taaluma hadhi katika jamii miongoni mwa makundi mengine. Utafiti huu umejikita kwenye suala la uana hasa kwa kutathmini jinsi taswira dumifu zinavyodhihirika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Uhakiki mwingi wa kazi za fasihi ya Kiswahili kuhusiana na maswala ya uana umeonekana kujikita na kuegemea katika kazi zilizodhamiriwa kusomwa na wasomaji wapevu. Tafiti za aina hii zimefanywa katika tanzu za ushairi, riwaya, hadithi fupi,

tamthilia na fasihi simulizi. Utafiti wa aina hiyo katika kiwango cha fasihi ya Kiswahili ya watoto haujashughulikiwa sana. Utafiti huu umechochewa na hali hiyo. Isitoshe watunzi wa fasihi ya watoto ni watu wazima ambao hujaribu kuwasawiria watoto ulimwengu kwa kutumia darubini za utu uzima kuupima ulimwengu wa watoto.

Tunaamini kwamba, fasihi ya Kiswahili ya watoto kama zao la jamii ni nyenzo muhimu ambayo kupitia kwayo watoto wanaweza kukumbana na wahusika na matukio wanayoweza kujitambulisha na kujinasibisha nayo. Wahusika na matukio katika fasihi hiyo huwakaribisha watoto kuweza kuuona ulimwengu kupitia kwa macho ya wengine na kuwapa fursa ya kujenga mitazamo yao binafsi na ulimwengu mpana.

Uana ni kile ambacho watu hufikiria kuhusu kuwa ama mwanamke au mwanaume. Mielekeo na mienendo hii hubwiwa kutokana na jamii husika na tamaduni ambamo watu hukulia. Utafiti huu unachunguza namna watoto wa jinsia za kike na kiume husawiriwa katika fasihi ya Kiswahili ya watoto hasa kwa kuangazia kipengele cha taswira dumifu za uana.

Taswira dumifu za uana katika fasihi ya watoto zinaweza kuwa tatizo maalum kwa sababu ya uwezo wa kuathiri mtagusano wa kijinsia na hivyo basi kupenyeza kwenye mtazamo wa watoto kujihusu wao wenyewe na watu wengine. Aidha baadhi ya taswira dumifu huwakweza hadhi watoto wa jinsia moja na kuwadunisha watoto wa jinsia nyingine.

## 1.1 Somo la Utafiti

Utafiti huu ni uhakiki wa taswira dumifu za uana kama zinavyojitokeza katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti huu unakusudia kumulika jinsi taswira hizo zinavyosheheni ubaguzi wa kijinsia. Ili kubainisha ubaguzi huo, utafiti huu unaangaza jinsi waandishi wa fasihi ya watoto ya Kiswahili wanavyowasawiri wahusika wao, jinsi wanavyowapa majukumu na jinsi wanavyosawazisha majukumu hayo baina ya wahusika wa kike na wa kiume.

Suala la usawa wa idadi ni suala la kimsingi katika utafiti huu kwa sababu linamulika uhalisi uliopo katika fasihi hii. Aidha wasomaji hujitambulisha na kujinasibisha na wahusika wa jinsia zao kwenye fasihi. Ukosefu wa wahusika wa jinsia ya kike au kiume kwenye matini ya fasihi ya watoto kwa mfano kunaweza kuwanyima hadhira hiyo ya wasomaji fursa ya kujinasibisha na kujitambulisha na jinsia zao na kutambua nafasi zao katika jamii husika.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Uhalisia uliopo katika fasihi ya Kiswahili ya watoto ni kwamba waandishi wa fasihi hii hawazingatii usawa wa kijinsia wanapotunga kazi hizo. Hali hii huzua matokeo ambapo kazi hizo ama zina wahusika wa jinsia moja na iwapo wahusika wa jinsia zote wamewakilishwa, jinsia moja imebaguliwa kwa misingi ya taswira dumifu za uana.

Utafiti huu unalenga:

(i) Kuchunguza ni kwa kiwango na kwa namna gani waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wanaendeleza taswira dumifu za uana zinazoendeleza ubaguzi wa kijinsia. Je, uendelezaji huu ni jambo linalofanywa kimaksudi au ni sadfa?

(ii) Kutathmini iwapo wahusika wa kike na wa kiume katika fasihi ya watoto wamesawiriwa kwa usawa au iwapo wamebaguliwa kwa misingi ya jinsia zao. Lengo kuu la madhumuni haya ni kuonyesha kwamba kutosawiriwa kwa wahusika kwa njia ya usawa katika fasihi ya watoto kunaweza kuchangia katika kuendeleza taswira dumifu za uana katika jamii husika.

## 1.3 Nadharia tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete kwamba:

i) Taswira dumifu za uana zinadhihirika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

ii) Wahusika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto husawiriwa kwa njia sawa bila kubaguliwa kwa misingi ya jinsia yao.

iii) Waandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili ya watoto huwakilisha idadi sawa ya wahusika wa jinsia ya kike na kiume.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Somo Hili

Utoto ni awamu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Ni katika awamu hii ambapo watoto hujifunza kutoka kwa wenzao, wazazi wao, vyombo vya habari kama vile redio, runinga na usomaji wa fasihi kwa jumla. Wataalamu wa maswala ya saikolojia ya watoto wameonyesha kwamba ukongomelevu (fixation) wa tabia za mtu mzima zina chanzo chake utotoni. Tunaamini kwamba ubwiaji wa taswira dumifu za uana kutokana na fasihi ya watoto ya Kiswahili unaweza kuchangia hali hii na hivyo basi pana haja ya waandishi kudhibiti taswira hizo. Wahakiki waliotangulia katika uwanja huu hawajaitilia maanani fasihi ya Kiswahili ya watoto. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hili.

Sababu ya pili ya kuchagua somo hili ni kuwa taswira dumifu za uana katika fasihi ya watoto zinaweza kuwa tatizo la kijamii kwa sababu ya uwezekano mkubwa wa taswira hizo kuathiri matangamano ya uana, maoni na mitazamo ya watoto kujihusu wao wenyewe na watu wengine katika jamii. Nchini Kenya ambapo Kiswahili ni somo la lazima katika viwango vyote vya mfumo wa elimu - isipokuwa vyuo vikuu, uwezekano wa watoto kubwia taswira dumifu hasi kupitia fasihi ya Kiswahili ya watoto ni mkubwa.

Sababu ya tatu ni kwamba, fasihi ya watoto ni eneo lililopuuzwa katika idara za fasihi katika vyuo vikuu kote ulimwenguni, (Indangasi, 2006: iv) Tunakubaliana na kauli hii kwa misingi kwamba, inapotokea kuwa fasihi hii inafundishwa katika taasisi za elimu na hasa vyuo vikuu, wanafunzi huichukulia kuwa 'fasihi ya kitoto'. Aidha kuna uwezekano kuwa watu huhoji busara iliyoko katika kuwafundisha watu wazima fasihi ya watoto.

Kuna basi dharura ya kufanywa tafiti nyingi katika utanzu wa fasihi ya watoto kwa sababu hali ya baadaye ya vijana wetu na kwa hakika jamii yetu itategemea aina ya fasihi ya watoto inayosomwa na watoto wetu. Utanzu wa fasihi ya watoto huonwa kwa ujumla kuwa utanzu ulio pembezoni na usiokuwa na mvuto wowote unaoweza kuwavutia wasomi licha kwamba fasihi hii hutoa mchango mkubwa kama chombo cha kuelimisha, kuburudisha na kuendeleza itikadi za jamii husika (Puurtinen, 1998). Kuna misururu ya vitabu vingi vya fasihi ya watoto vinavyochapishwa kila mwaka na hali havihakikiwi. Katika kufanya tahakiki kama hii, tunaamini kwamba tunatoa mchango katika kuziba pengo hilo.

## 1.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Katika utafiti huu, tumedurusu aina mbili za maandishi; maandishi kuhusu maswala ya uana na maandishi kuhusu fasihi ya watoto.

### 1.5.1 Maandishi Kuhusu Maswala ya Uana

Tahakiki za maswala ya uana katika kazi za fasihi ya Kiswahili zilianza hasa katika miaka ya katikati ya mwongo wa kuanzia 1980 (King'ei, 2002). Tangu wakati huo mpaka sasa, tafiti nyingi kuhusu maswala ya uana zimefanywa katika tanzu za ushairi, riwaya, tamthilia, hadithi fupi na fasihi simulizi. Hatufahamu utafiti wowote uliokwisha kufanywa kuhusu maswala ya uana katika utanzu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Hali hii inaashiria kwamba ama utanzu huu umepuuzwa au wahakiki hawatambui kukua kwake hadi sasa. Utanzu wa fasihi ya watoto na hasa katika Kiswahili umepiga hatua kubwa tangu wakati kabla ya ukoloni ambao ulitawaliwa na fasihi simulizi, kipindi cha

ukoloni ambacho kilitawaliwa na fasihi andishi iliyosheheni itikadi za kikoloni na fasihi ya kipindi baada ya uhuru ambapo tunapata kazi nyingi zilizotungwa na waandishi wa Kiafrika na hata katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili (Odaga, 1985:1-21).

Katika makala yake 'The Images of Women in Tanzanian Oral Literature' (1982) Balisidya Matteru amezungumzia swala la taswira za mwanamke katika fasihi simulizi ya Tanzania. Maoni yake ni kwamba dhiki zinazowakumba wanawake huletwa na mahusiano mabaya ya kijamii kati ya wanawake na wanaume. Uchunguzi wa Matteru hauonyeshi chanzo cha mahusiano hayo mabaya. Utafiti wetu umepiga hatua katika kudadisi ni kwa vipi fasihi ya Kiswahili ya watoto, kama mojawapo ya nyenzo za mtagusano katika jamii inachangia taswira dumifu za uana ambazo hatimaye huathiri mahusiano kati ya wanawake na wanaume anaowazungumzia Matteru. Kwa usemi mwingine, wanawake na wanaume hupitia awamu ya utotoni kabla ya kufikia ngazi hiyo. Je, kuna uwezekano kuwa mahusiano yao mabaya huchangiwa na usomaji wa fasihi yenye taswira dumifu za uana utotoni mwao? Ingawa utafiti wa Matteru umejikita katika fasihi simulizi, maoni yake yametufaa katika utafiti huu kwa sababu kazi hizi mbili zinajishughulisha na masuala ya uana.

Aidha, tahakiki ya Patricia Mbughuni, 'The Image of Women in Kwahili Prose Fiction' (1982:15-24) inajadili taswira za wanawake katika riwaya za Kiswahili za Tanzania. Mbughuni anasema kwamba, taswira mbaya za mwanamke zinatokana na sababu kwamba tungo hizo zimeandikwa na wanaume. Tahakiki hii imeegemea upande mmoja kwani inatathmini fasihi iliyoandikwa na waandishi wa kiume. Ili kupata picha halisi jinsi

mwanamke anavyosawiriwa katika kazi za kifasihi, ipo haja pia kuchunguza kazi zilizoandikwa na waandishi wa kike. Utafiti wetu unaziba pengo hili kwa sababu unahakiki kwa pamoja kazi za waandishi wa kike na wa kiume, ila tu utafiti wetu unachunguza taswira dumifu za uana katika kazi hizo.

Katika tasnifu yake, 'Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria' Catherine Ndungo (1985) amechunguza jinsi sura ya mwanamke inavyobadilika kutokana na mapito ya wakati. Mtazamo huu wa kihistoria unachukua msimamo wa Kimaksi kwamba ukombozi wa mwanamke wa tabaka la chini linalodhulumiwa unatokana tu na kuangushwa kwa mfumo wa kijamaa unaosisitiza usawa wa kiuchumi na kisiasa. Madhumuni ya uchunguzi wa Ndungo ni kubainisha jinsi mabadiliko ya kihistoria yanavyowaathiri wanawake. Ndungo kwa ujumla anaangazia maswala ya uana katika kazi zilizodhamiriwa kusomwa na hadhira ya wasomaji wapevu. Utafiti tunaoufanya unahusu taswira dumifu za uana katika fasihi iliyodhamiriwa hadhira ya wasomaji chipukizi. Fikra za Ndungo zimetufaa kwa kiasi fulani kwa sababu utafiti wake umegusia mambo tunayojishughulisha nayo ingawa katika muktadha tofauti.

Makala ya chacha Nyaigotti Chacha (1986) 'Mazingira ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili: Rosa Mistika wa E. Kezilahabi' yanabainisha kuwa, mhusika, Rosa hafai kuhukumiwa ila kuhurumiwa kwa sababu ni mdhulumiwa wa jamii kongwe isiyoelewa mfumo wa maisha ya kisasa. Riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) ni riwaya ambayo kimsingi inaangazia athari za malezi mabaya kwa watoto, hasa watoto wa kike. Chacha anaonekana kuwa kimya kabisa kuhusu mchango wa malezi mabaya ya kifamilia katika

maisha ya baadaye ya Rosa. Kuwaelimisha watoto ni mojawapo ya majukumu ya wazazi katika malezi. Utafiti huu unajikita kwenye machukulio kwamba usomaji wa fasihi miongoni mwa watoto wanapoelimishwa kunaweza kuchangia katika kukongomelea baadhi ya taswira dumifu za uana ambazo zinaweza kumwathiri mtu katika utu uzimani.

Kwenye tasnifu yake 'Women in African Drama Representation and Role' Ciarunji Chesaina, (1987) amechunguza usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia zilizoandikwa kwa Kiingereza na Kifaransa. Chesaina amewalinganisha waandishi wa kike na kiume. Amebainisha kwamba, waandishi wa kike wanatofautiana kwa kiasi kikubwa na waandishi wa kiume kwa jinsi wanavyowasawiri wahusika wa kike. Anahoji kwamba wanaume wanapoandika kuhusu wanawake hawaelezei dhiki zao kwani hawajakumbana na dhiki na dhuluma za aina hiyo na hivyo hawana tajriba zozote za kuwawezesha kuelezea hali halisi ya wanawake. Tofauti ya utafiti wa Chesaina na huu wetu, ni kwamba amejishughulisha na utanzu wa tamthilia huku tukijishughulisha na fasihi ya watoto. Ingawa tunachota data yetu kutoka kwa kazi za fasihi ya watoto zilizotungwa na wanaume na wanawake, utafiti wetu haufanyi ulinganisho wowote kuhusu taswira dumifu za uana katika vitabu vilivyoandikwa na waandishi wa kike na vile vilivyoandikwa na wandishi wa kiume bali unaonyesha jinsi taswira hizo zinavyobainika na ni kwa vipi zinaendeleza ubaguzi.

Dhana kuwa mwanamke amefanywa kinyago na chombo cha kumtumikia mwanamume imetiliwa nguvu katika tafiti kadhaa (Abdulaziz, 1979, Imbosa, 1990). Watafiti hawa wameuchambua ushairi wa Muyaka Bin Haji (1776-1840) unaomwakilisha mwanamke

kama kiumbe anayemtegemea mwanamume kwa kila hali ili maisha yake yaweze kukamilika. Tafiti za wataalamu hawa zimetufaidi kwa kiasi fulani kwa sababu tunachunguza iwapo taswira dumifu ya utegemezi wa wahusika wa kike kwa wahusika wa kiume ni miongoni mwa taswira tunazochunguza iwapo zinajitokeza katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Mbali na ushairi, kazi za nathari pia zimekwisha kutafitiwa katika kipengele cha maswala ya uana. Utafiti uliokwisha kufanywa katika eneo hilo ni pamoja na wa Lughano Rose (1989) na Muindi (1990) ambao wamehakiki riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Muindi amechunguza kwa undani maudhui ya ukahaba na kuhitimisha kwamba hili ni swala la kiuchumi na mwanamke hushawishika kujihusisha na biashara hiyo kwa sababu jamii iliyotawaliwa na mwanamume inamwonea. Muindi anachota data yake kutoka kwa riwaya ya *Utengano*. Aidha kutokana na utafiti wake, Lughano ametoa kauli kwamba Kezilahabi ni mwandishi anayeegemea nadharia ya utamaushi na pia mzingatifu wa taasubi ya kiume. Kwa hivyo, haoni uwezekano wowote wa kujikomboa kwa mwanamke kutokana na maonevu ya jamii yake. Kulingana na Lughano, Kezilahabi anawafungamanisha wahusika wake wa kike pamoja na wanyonge wote wa jamii ambao daima dawamu watabakia katika hali yao ya mateso.

Ingawa tafiti za Lugano na Muindi zinatofautiana na wetu kwa sababu zimejikita katika riwaya ya Kiswahili, ni msingi mzuri ambao umetusaidia kutathmini iwapo mhusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili ya watoto amesawiriwa kwa njia inayodhihirisha taswira

dumifu ya uana ya unyonge huku mwenzake wa kiume akisawiriwa kuwa mwenye nguvu na mamlaka.

Katika utanzu wa tamthilia, utafiti kuhusu swala la uana umefanywa na Katwiwa Mule (1991). Mule amehakiki tamthilia za *Zinduko* ya Sheilla Ryanga (1986) na *Mama Ee* ya Ari Katini Mwachofi (1987). Kutoka Tanzania, Mule amechunguza tamthilia za Penina Muhando na Chogo. Mtafiti huyu ameafiki maoni ya watafiti waliomtangulia kwamba mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni na mtegemezi wa mwanamume.

Tafiti nyingine zilizokwisha kufanywa kuhusu taswira za mwanamke katika kazi za fasihi ya Kiswahili ambazo zimeufaa utafiti wetu ni pamoja na John Kiango (1992), Wanjiku Kabira (1993 & 1994). Kiango ameshughulikia taswira za mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Amebainisha kwamba taswira za mwanamke katika tamthilia za Kenya ni nyingi lakini mkabala wa taswira hizo unatokana na waandishi wa kazi hizo kutomwangalia mwanamke katika mfumo wa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kumpa nafasi yake anayostahiki. Katika utafiti wetu, tunachunguza kubainisha iwapo kuna taswira dumifu za uana zinazombagua mtoto wa jinsia ya kike anapolinganishwa na mwenzake wa kiume.

Kabira (1993& 1994) naye amehakiki taswira za mwanamke katika ngano za Wagikuyu. Miongoni mwa taswira za wanawake anazobainisha kujitokeza katika ngano hizo ni pamoja na wanawake kusawiriwa kuwa waongo, wasio waaminifu na wasio wazalendo.

Anasema kuwa, kwa namna hii, kunaendelezwa utawala wa bwana kwa bibi kwa jumla hivyo basi kuunga mkono kunyanyaswa kwa wanawake. Anatoa mwito wa kuchunguzwa upya utambaji wa ngano hizo ili kuelewa barabara ukosefu wa usawa wa kiuana katika muktadha wa Afrika mbali na kubuni utamaduni unaoleta usawa wa kiuana. Utafiti wa Kabira umetufaa katika kuangazia hali ya ukinzani kuhusu majukumu wanayopewa watoto wa jinsia ya kike na kiume katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Katika utanzu wa fasihi simulizi utafiti kuhusu swala la uana umefanywa na Catherine Ndungo. Katika tasnifu yake, 'Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Kiswahili na Agikuyu' (1998) ameonyesha kuwa utamaduni na malezi huchukua nafasi muhimu katika kuunda na kuimarisha itikadi na mielekeo ya jamii kuhusu wanawake. Utafiti wa Ndungo unaingiliana kwa kiasi na huu tunaoufanya ila wetu unasisitiza mielekeo ya jamii kuhusu watoto wa jinsia za kike na kiume hasa kwa kuzingatia swala la taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Katika utafiti wake, 'Artistic Choices And Gender Placement in The Writings of Ngugi wa Thiongo And Grace Ogot' Evan Mwangi (2002) anachunguza iwapo waandishi wa kike na wa kiume hutumia lugha na usimulizi tofauti kwa mintaarafu ya uana wao. Mwangi anawalinganisha waandishi wawili – Ngugi wa Thiong'o na Grace Ogot huku akitathmini iwapo mitindo tofauti ya vipengele hivyo inaweza kuelezewa kwa kuegemea jinsia ya wasanii husika. Kadhalika, utafiti wa Mwangi unachunguza jinsi wasanii hao wanavyowasawiri wahusika wa kike na kiume katika kazi zao. Utafiti huu umetufaa kwa sababu uchunguzi wetu unalenga kubaini jinsi wahusika wa kike na wa kiume

wanavyosawiriwa katika kazi za kubuni zinazolenga watoto ili kuonyesha taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Makala ya Momanyi (2002), 'Swala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili' yamejadili na kutalii swala la nadharia badilia ya Kiafrika itakayoweza kushughulikia fasihi za Kiafrika, ikiwemo fasihi ya Kiswahili, mbali na kuainisha vigezo vinavyoweza kutumiwa ili kuteua nadharia kama hiyo. Anahoji kwamba lengo la nadharia hii ni kuifufua na kuirutubisha sauti ya mwanamke wa Kiafrika iliyofichwa na dahari nyingi za mamlaka ya kiume. Makala haya ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yanatupa mwongozo kuhusu nadharia ya ufeministi ambayo ni mojawapo ya nadharia inayoongoza utafiti huu.

Aidha, Momanyi (1999) na Matundura (2003) wamezungumzia swala la kubaguliwa kwa mtoto wa kike na baadhi ya tamaduni za Kiafrika. Kwa mujibu wa Momanyi, asasi za kijamii kama vile familia, shule, dini na jamii pana zina mchango mkubwa katika kumkabidhi mtu funguo za elimu na maarifa. Endapo mtoto wa kike atanyimwa nafasi ya kuelimika basi, jamii inayomkuza haina budi kulaumiwa. Kwa hivyo, kwa mujibu wa Momanyi, tangu pale anapozaliwa, mtoto wa kike anastahili kupokea maadili yatakayomwongoza kuipenda na kuithamini nafsi yake kama kiumbe aliyekamilika. Makala ya Momanyi na Matundura ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yanamulika masuala ya watoto wa jinsia ya kike na ya kiume. Yameufaa utafiti wetu kwa sababu baadhi ya taswira dumifu za uana zinazochunguzwa katika vitabu vya fasihi ya Kiswahili

zinalenga kubainisha iwapo waandishi wa kazi hizo wamedumisha usawa miongoni mwa wahusika au wamebagua watoto wa jinsia moja na kuwakweza wa jinsia nyingine.

Uchunguzi wa Wafula 'Gender Relations in Ben Okri's Trilogy: *The Famished Road, Songs of Enchantment & Infinite Riches*' (2004) umeangazia mahusiano ya kijinsia katika riwaya tatu za Ben Okri. Riwaya hizi ni pamoja na *The Famished Road, Songs of Enchantment* na *Infinite Riches*. Wafula ametathmini jinsi majukumu ya wanawake na wanaume yanavyoathiri matangamano yao na umma mpana. Kadhalika, utafiti huu umeshughulikia miundo ya mwegemeo wa kuumeni katika jamii (patriarchal constructs). Utafiti huu umeifaa kazi hii kwa sababu umejishughulisha na masuala ya uana na majukumu ya wahusika kwa misingi ya jinsia yao. Tofauti ya utatiti wa Wafula na huu wetu ni kwamba, huku Wafula akitumia nadharia kijamii (social theory) utafiti wetu umenufaika na mikabala ya uana na ufeministi kwa kiharakati.

### 1.5.2 Maandishi kuhusu Fasihi ya Watoto

Hakuna chochote kilichoandikwa kuhusu swala la taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Hata hivyo, kuna maandishi kadha wa kadha yaliyoandikwa kuhusu fasihi ya watoto kwa jumla. Gachukia na Akivaga (1978) wameangalia kwa jumla fasihi ya watoto nchini Kenya.Wataalamu hawa wameonyesha jinsi kazi za Wazungu zilimwathiri Mwafrika kimawazo. Ingawa mkabala wa utafiti wa wataalamu hawa ni tofauti na wetu, mawazo yao yametufaa kwa kuwa wamejadili kipengele cha jinsi fasihi inaweza kuathiri watu. Utafiti wetu unaangazia jinsi watoto wanaweza kuathiriwa na taswira dumifu za uana wanazokumbana nazo katika fasihi ya watoto.

Hellen Oronga Mwanzi (1982) amechunguza fasihi ya watoto nchini Kenya na nafasi ya fasihi hiyo katika kuchangia maendeleo ya utamaduni na maadili ya kijamii. Uchunguzi wa Mwanzi umejikita kwenye uhusiano uliopo kati ya taswira katika vitabu vya fasihi ya watoto na ruwaza ya mienendo (behaviour patterns) ya watoto wanaoisoma fasihi hiyo. Mwanzi anashughulikia taswira kwa ujumla ilihali tunafahamu kwamba kuna aina nyingi za taswira, hasi na chanya. Mwanzi anasema kwamba kila mwandishi wa fasihi ya watoto huandika kwa lengo la kuathiri mwonoulimwengu wa watoto kuhusu jamii yao. Utafiti huu unapiga hatua kwa kuangazia taswira mahususi, taswira dumifu za uana.

Asenath Bole Odaga (1985) ameshughulikia hadithi za kubuni za watoto nchini Kenya. Ameangalia vipindi vitatu vya kihistoria vya fasihi ya watoto; kipindi kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni na kipindi cha baada ya ukoloni. Licha ya mchango wake, kuangalia fasihi ya watoto katika vipindi vitatu kwa mkupuo mmoja ni kazi kubwa ambayo kwa sababu ya upeo wa aina hiyo, mtafiti hawezi kuangazia kikamilifu maswala yote muhimu. Kwa sababu hii, Odaga amegusia kijuujuu kila kipindi bila kuzama kwa kina. Utafiti wetu umejikita kwenye fasihi ya watoto iliyochapisha katika kipindi cha baada ya ukoloni. Kazi zinazoshughilikiwa zimechapishwa kati ya mwaka 2001 – 2006.

Utafiti kuhusu vitabu vya fasihi vinavyosomwa na watoto umefanywa na Akoilet (1990) na Weche (2000). Weche amevihakiki vitabu vya Ezekiel Alembi huku akiangazia jinsi fasihi ya watoto inaweza kuwa kioo cha kumwongoza mtoto kitabia. Akoilet amevihakiki vitabu vya Barbara Kimenye ambapo ameshughulikia upokezi wa fasihi ya watoto. Tafiti

hizi, hasa utafiti wa Weche umeufaa utafiti huu kwa sababu ya umeshughulikia swala la fasihi ya watoto kumwathiri mtoto na kumwongoza kitabia.

Utafiti wa Nyambura Mpesha (1995) ambao umeshughulikia ukuaji wa fasihi ya watoto nchini Tanzania umeufaa utafiti huu kwa kuwa umetoa mwelekeo wa jinsi fasihi ya watoto huathiriwa na mapisi ya wakati. Watafiti wengine ambao tafiti zao zimeufaa utafiti huu ni pamoja na Alembi (1991) na Okhoba (1995) ambao wameshughulikia fasihi simulizi ya watoto na utanzu wa ushairi.

Fidelis Muthubi (2005) ameshughulikia swala la mikakati na mbinu za usilimishwaji katika fasihi ya watoto. Mtafiti huyu amehakiki riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (Matundura, 2001), *Mashimo ya Mfalme Suleman* (Johnson, 1981) na *Alfu Lela Ulela* [(Kitabu cha Pili) Brenn, 1962]. Uchunguzi huu umeufaa utafiti huu kwa sababu umeangazia kwa mapama wahusika. Utafiti huu unajishughulisha na taṭhmini ya taswira dumifu za uana kwa kuwaangazia wahusika na majukumu waliyotengewa katika kazi tunazozihakiki.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Swala la uana ni pana sana na linaweza kuchunguzwa kwa kuzingatia mikabala mingi; uana na elimu, ajira, ardhi na kilimo, biashara na sekta isiyokuwa rasmi, siasa na maamuzi ya umma, uana, katiba na sheria, dhuluma na mizozo, ndoa, mazingira, urathi, haki ya matangamano kwa kutaja tu mikabala michache. Utafiti huu umejikita kwenye

suala la uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto hasa katika kutathmini jinsi fasihi hiyo inavyoakisi taswira dumifu za uana.

Fasihi ya Kiswahili ni pana mno kwa sababu imetanda vipindi vitatu virefu vya kihistoria. Odaga (Khj) amevigawa vipindi hivyo ifuatavyo: kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Utafiti huu umechota data yake kutoka kwa fasihi ya kipindi cha baada ya ukoloni, hasa kazi zilizochapishwa katika kipindi kimoja. Kazi zinazohakikiwa zimechapishwa baina ya miaka 2001 na 2006. Tumeteua kazi za kipindi kimoja kwa sababu muda uliotengewa utafiti huu ni mfupi mno na hauturuhusu kuhakiki kazi za vipindi tofauti.

Aidha tunahakiki kazi za fasihi ya watoto zenye wahusika binadamu. Watunzi wa fasihi andishi ya watoto mbali na kutumia wahusika binadamu pia hutumia hutumia wahusika wanyama, binadamu na wanyama, wahusika binadamu na mazimwi, miongoni mwa wahusika wengine. Utafiti huu umejikita kwenye kazi za kifasihi zenye wahusika binadamu kwa sababu wahusika binadamu wanakaribia uhalisia zaidi kuliko wahusika wanyama na mazimwi. Aidha ni rahisi kutambua jinsia za wahusika binadamu kutokana na majina yao, tofauti na wahusika wanyama.

Mojawapo ya sifa za kimsingi za fasihi ya watoto ni kwamba huandamana na michoro au picha. Utafiti huu unachunguza taswira dumifu za uana kama zinavyobainika katika matini za kimaandishi na wala sio matini za michoro. Ingawa michoro ni sehemu ya matini (paratext), mara nyingi katika fasihi ya watoto, mwandishi huwa siye mchoraji wa

picha kwenye vitabu hivyo. watoto. Isitoshe, mchoraji anaweza kushindwa kufasiri matini ya mwandishi na hivyo basi kupotosha ujumbe wa mwandishi. Matini tunazozichunguza kwenye utafiti huu ni pamoja na za waandishi wa kiume (androtexts) na matini za waandishi wa kike (gynotexts). Tumefanya uteuzi wa aina hizi za matini kimaksudi ili kudumisha usawa wa kiuana – hasa tukizingatia kuwa utafiti huu unahusu maswala ya taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Kazi ambazo tumezihakiki katika utafiti huu ni pamoja na; *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* (K.W. Wamitila, 2006), *Mgomba Changaraweni* (Ken Walibora, 2004), *Mwanasesere wa Mosi* (Demere Kitunga, 2002), *Siku ya Wajinga* (Clara Momanyi, 2005), *Ndoto ya Riziki* (Razwana Kimutai, 2003) na *Alitoroka Kwao* (Angelina Mdari, 2001).

**1.7 Njia za utafiti**

Utafiti huu kimsingi ni wa maktabani na umetoa data yake katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Utaratibu ambao tumeufuata katika utafiti huu pamoja na kuzigawa matini za fasihi ya Kiswahili ya watoto katika makundi mawili makuu: matini zilizoandikwa na waandishi wa kiume (androtexts) na matini zilizoandikwa na waandishi wa kike (gynotexts).

Baada ya kugawa kazi hizo katika makundi hayo, tumezisoma kwa makini na kutoa muhtasari wa kila hadithi, kisha tumedondoa sehemu za matini za hadithi zinazosheheni taswira dumifu za uana. Maswali ambayo yametuongoza katika kubainisha ni zipi taswira

dumifu za uana na ni zipi zisizo taswira dumifu za uana yametokana na mikabala ya ufeministi wa kiharakati na uana ambayo imeongoza utafiti huu. Maswali hayo ni pamoja na: Je, mwandishi ni wa kike au ni wa kiume? Wahusika wa kiume wana majukumu gani na utendaji upi kwenye matini? Wahusika wa kike wamepewa nafasi gani – ni wahusika wakuu au ni wahusika wajenzi? Je, wahusika wa kiume wana mielekeo ipi kuhusu wahusika wa kike? Wahusika wa kike wana mielekeo ipi kuhusu wenzao wa kiume? Miongoni mwa wahusika wa kike na kiume, ni nani anayemsaidia mwenzake na ni msaada wa aina gani? Ni mhusika wa jinsia gani mwenye mamlaka?

Kadhalika, tumeegemea vifaa vya kuchezea, masomo shuleni, sifa bainifu za kibinafsi na taaluma za wahusika wa kike na kiume kwenye dondoo za matini ya kazi tunazohakiki kubainisha taswira dumifu za uana. Uchanganuzi wa data kuhusu taswira dumifu za uana umefanywa kwa njia ya mjadala huku tukitoa ushahidhi kutoka kwenye matini husika kwa kusisitiza au kunukuu wataalamu wa fasihi nje ya matini husika kushadidia hoja zetu.

Hali kadhalika tumehesabu idadi ya wahusika wa kila jinsia katika kila matini ya hadithi ili kubainisha swala la uwakilishi kiidadi wa wahusika wa jinsia ya kike na kiume. Ili kuzuia mahitimisho yasiyokuwa ya kihisia, utafiti huu umenufaika na majadiliano na wataalamu wa fasihi, wasimamizi wa kazi hii na baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi zilizohakikiwa. Majadiliano ya aina hiyo yamezuia kutokuwepo kwa upendeleo katika utafiti huu.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na mikabala miwili ya kiuhakiki; mkabala wa kiuana na mkabala wa ufeministi wa kiharakati.

Mkabala wa kiuana ni mkabala unaojishughulisha na masuala ya kimahusiano katika jamii. Mahusiano haya kwa kawaida yanajibainisha katika misingi mbalimbali ikiwemo, mahusiano ya kijinsia, mahusiano ya kitamaduni, mahusiano ya kiutenda kazi, mahusiano ya ki-asasi n.k. Madai haya yanatusaidia sio tu kumulika na kuangazia uhalisi wa jamii, bali pia aina za uhalisi huo, misingi yake pamoja na athari zake.

Nao mkabala wa ufeministi ni mkusanyo wa 'nadharia' nyingi ambao kimsingi lengo lake ni kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume. Wahakiki wanaoegemea mkabala huu wanashikilia msimamo kwamba ulimwengu unaoaminika kutawaliwa na wanaume unahitaji mabadiliko baina ya watu wote, tamaduni zote na kwamba watu wa jinsia zote wanapaswa kuthaminiwa.

Tofauti ya kimsingi iliyoko kati ya mikabala hii ni kwamba mkabala wa kiuana ulichipuza kutokana na ufeministi ambao kama ambavyo tumekwisha kutaja hapo juu sio nadharia moja bali mkusanyo wa mikabala mbalimbali. Ufeministi wa kiharakati ni mojawapo ya mikabala ya ufeministi mpana. Kimsingi, ufeministi ni mkabala wa wanawake hasa katika mataifa ya Kimagharibi. Akipinga matumizi ya nadharia na mikabala ya Kimagharibi katika shughuli za uhakiki wa kazi za kifasihi za Kiafrika; Oyeronke Oyewumi (1997: ix) anasema:

> Swala la mwanamke ni fikra iliyokopwa kutoka magharibi.
> [....]Halina asili yake katika jamii ya Wayoruba wala jamii

> nyingine nyingi za Kiafrika. Uhakiki wa kiusomi unaotegemea nadharia na mijadala ya dhana iliyoibuka na kutawala katika mataifa ya Kimagharibi, haiwezi kufumbata hali halisi katika jamii za Kiafrika.
>
> (Tafsiri Yangu)

Tunakubaliana na kauli ya Oyewumi. Kutokana na tahakiki mbalimbali zinazozidi kuongezeka kuhusu maswala ya uana, ni wazi kwamba ipo haja ya kuziendeleza tamaduni za Kiafrika na kuzitafakari ili zitupe suluhisho kuhusu nadharia ifaayo/zifaazo kushughulikia fasihi za Kiafrika. Lakini kwa sababu suluhisho la aina hiyo halijapatikana, uhakiki hauwezi kukwama kwa sababu ya kutokuwepo kwa nadharia badalia. Kwa hivyo, katika utafiti wetu, tunaegemea mkabala wa kifeministi ila kwa tahadhari hadi pale tutakapoibua nadharia zetu.

### 1.8.1 Mkabala wa Uana

Mkabala wa uana huangazia fasili za maswala ya utambulisho wa jinsia. Wafuasi wa mkabala wa uana wamejikita kwenye mawazo ya Jacques Lacan ya kuona jinsia na uana kama dhana kinzani, moja ni asilia (natural) huku nyingine ikiwa si asilia (artificial). Tulivyokwisha kutaja, jinsia ni maumbile ya kibaolojia na utambulisho wa ama kuwa kike au kiume. Uana kwa upande mwingine ni muundo wa jamii (social construct) unaotegemea taswira dumifu kutilia nguvu majukumu yaliyoamuliwa na jamii.

Mkabala wa uana ulichipuka kutokana na migogoro ya kihakiki katika ufeministi lakini ikakua sambamba na ufeministi katika miaka ya themanini na tisini. Ingawa mkabala wa uana huangazia pakubwa historia ya tamaduni, hutumiwa kufafanua kwa undani filamu pendwa na kazi za kifasihi kama vyombo vya kiutamaduni; na katika kufanya hivyo, mkabala huu unabainishwa na uwekaji alama baina ya maswala ya uana na jinsia.

Katika fasihi, mkabala wa uana mwanzoni ulijitokeza kama mawazo makuu ya ufeministi. Kwa mfano, uhakiki wa kazi zilizoandikwa na wanawake (gynocriticism) ulianzishwa na Elaine Showalter mwishoni mwa miaka ya sabini na ulilenga kubaini kwamba waandishi wa kike wana mtindo wao wa kuandika unaotofautiana na mtindo wa waandishi wa kiume. Tatizo kuu la mtazamo huu ni kuwa ulitilia nguvu wazo la uegemezi wa kuumeni, kwamba sifa za ndani za kiuana ni za kiuasilia kutegemea jinsia.

Wahakiki kama vile Julia Kristeva walitumia maoni ya Lacan kuchunguza na kutoa maelezo kuhusu vipengele vya utambulisho kama vile uana na jinsia kuwa na 'ruwaza ya lugha na mienendo ya kijamii' ambayo kutokana na kurudiwarudiwa inakua na kujikita na hatimaye kukubalika kama sehemu ya utamaduni. Kama vile tahakiki nyingine za kijamii zilizoibuka mnamo miaka ya sitini na sabini, nadharia ya uana ni chombo cha kisiasa. Wahakiki wa kiuana huchunguza majukumu ya wahusika kuzingatia jinsia zao. Iwapo wahakiki watapuuza uana, umma unaweza kushindwa kuelewa kwamba uana ni chombo ambacho kama vile lugha, kinatumika kuleta utaratibu na kuidhibiti jamii.

Katika kutathmini uana kwenye matini za kifasihi, wahakiki wanapania kudhihirisha kwamba, fasihi haiakisi tu utamaduni bali pia ni nyenzo ya kuusheheni na kuupitisha utamaduni huo. Fasihi huchangia katika kutilia nguvu viwango vya kitamaduni vya uana na jinsia. Kwa sababu hii, masuala kuhusu uana yanapaswa kuangaziwa na kutambuliwa – ndiposa pawe na uwezekano wa kufanya mabadiliko katika matarajio ya utamaduni.

### 1.8.2 Ufeministi

#### 1.8.2.1 Uibukaji na Maendeleo ya Kihistoria

Ufeministi ni mkabala unaotumiwa kuelezea mojawapo wa mkusanyo wa nadharia za kiuhakiki ambazo zimeshika nguvu katika miaka ya hivi karibuni. Ufeministi hujumlisha mikabala mbalimbali ya kiuhakiki ambayo licha ya tofauti zake, inaelekea kukubaliana au kuafikiana kwenye masuala kadha na malengo yake ya kimsingi kwamba mwanamke amekandamizwa na mwanamume kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Hivyo basi ufeministi umewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Ufeministi ni mkabala ambao unasaili na kudadisi misimamo na itikadi ya kiume ambayo imekuwako katika baadhi ya jamii ulimwenguni kwa kipindi kirefu. Huchunguza pia fasiri za kiume za fasihi pamoja na mikabala ya kibabedume. Ufeministi huzishambulia thamani za kiume katika fasihi kwa kuwashambulia waandishi wa kiume na uwasilishi wao wa wanawake na wakati huo huo kuwakweza waandishi wa kike.

Aidha, mkabala huu hujitahidi kufasiri uzoefu na tajriba za nafasi ya wanawake kama zinavyojitokeza katika tanzu mbalimbali za fasihi na hasa riwaya. Ufeministi pia hushambulia pia mitazamo ya kiume kuhusu jinsi wanawake wanavyopaswa kuhisi, kufikiri na kuitikia hali mbalimbali za kimaisha.

Baadhi ya kazi za kwanza zilizoamsha mwelekeo huu ni *A Room of One's Own View* ya Virginia Woolf (1882- 1941) ambaye alikuwa msomi kutoka Uingereza na *A Vindication of The Rights of Women* ya Mary Wollstonecraft. Hata hivyo, kazi inayochukua nafasi muhimu kinadharia ni kitabu cha Simone de Beauvoir (1908-1986) kijulikanacho kama *The Second Sex* (1949). Katika kitabu hiki, Beauvoir anashambulia baadhi ya asasi ambazo zinachangia katika ukandamizaji wa mwanamke. Asasi mbili kuu ni ndoa na utamaduni. Mwandishi huyu anazishambulia asasi hizi kwa kuelekea kumtazama mwanamke kwa njia hasi na kumwangalia kama 'wingine'. Anaishambulia mielekeo ya kiutamaduni ya kumfanya mwanamume kama kaida au binadamu kielelezo na kwa njia hiyo kuishia kumwangalia mwanamke katika misingi ya kiulinganishi tu. Kwa maoni ya de Beauvoir, utamaduni anamokulia mwanamke una mchango mkubwa katika kumdhalilisha na kumfanya hata aamini kwamba anapaswa kuikubali hali hiyo. Maoni haya yanasambazwa kutokana na mfumo wa ubabedume unaostawishwa katika jamii nyingi.

Ndoa kama asasi mojawapo ya utamaduni, inakuwa na mchango mkubwa katika kumdhalilisha mwanamke hasa kutokana na pingu inazomtia mwanamke. Suala la

mchango wa asasi hii katika maisha ya mwanamke linaendelezwa na mwanaufeministi wa kiharakati, Germane Greer katika vitabu vyake viwili *The Female Eunuch* na *The Whole Woman.* Katika kitabu cha kwanza, mwanaharakati huyu anaishia kupendekeza kwamba, wanawake wanapaswa kuisusia asasi hii inayowakandamiza kwa kutoolewa. Kwa kuolewa, mwanamke anageuzwa kuwa kitu cha kumilikiwa na kuwako kwake hufutwa.

Mwandishi mwingine ambaye amekuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa nadharia hii ni Kate Millet katika kazi yake *Sexual Politics (*1969*)* ambapo anazishambulia kazi za waandishi wa kiume kama Jean Genet, Norman Miller, Henry Miller na D.H. Lawrence. Kwa mujibu wa Millet, waandishi hawa wanamsawiri mwanamke kwa njia hasi katika kazi zao mbalimbali. Sababu kuu ya kufanya hivyo ni nia ya kuendeleza itikadi ya ubabedume. Katika kazi hii, Millet anaishambulia nadharia ya kisaikolojia inayohusishwa na Sigmund Freud kwa mchango wake mkubwa katika kuitilia nguvu itikadi hiyo.

Wahakiki wa baadaye kama Toril Moi katika *Sexual/Textual Politics* wanachunguza mitazamo ya uwili katika jamii. Uwili huu unajitokeza kwa kumhusisha mwanamume na sifa chanya ilhali mwanamke anahusishwa na sifa hasi. Katika miaka ya hivi karibuni, pamekuwepo na mielekeo ya kusisitiza usawiri chanya wa wahusika wa kike katika kazi za fasihi.

Tulivyotangulia kutaja, ufeministi sio nadharia moja. Hivyo basi, ni wananadharia wachache wakubalianao kuhusu mkabala mmoja wa ufeministi katika uchanganuzi wa

matini. Licha ya kuwepo hali hiyo, maeneo ya kijiografia huchangia pakubwa katika kubainisha sauti mbalimbali za uhakiki wa kifeministi. Kwa mujibu wa Charles E. Bressler (2003:150) ufeministi umenasibishwa na maeneo matatu ya kijiografia: Marekani, Uingereza na Ufaransa. Bressler hataji Afrika ambalo pia ni eneo la kijiografia lenye aina yake ya ufeministi. Wahakiki wa Kiafrika wanaojishughulisha na maswala ya uana wanaelekea kukubaliana kwamba mkabala wa ufeministi unaafiki zaidi uhakiki wa kazi za kimagharibi kuliko kazi za Kiafrika (Ogundipe-Leslie, 1994, Oyewumi, 1997, Steady, 1981). Hata hivyo, huku juhudi za kutafuta mkabala wa ufeministi unaoafiki uhakiki wa fasihi ya Kiafrika, hatuna budi kuegemea ufeministi wa kimagharibi ila kwa tahadhari huku tukichuja ni yepi ya kupokea na ni yepi ya kutupilia mbali.

Kulingana na Elaine Showalter, Ufeministi wa Kimarekani huangazia mno jinsi matini za kifasihi zinavyowakandamiza wanawake; ufeministi wa Uingereza umeegemea Umarx huku ufeministi wa Ufaransa ukiegemea saikolojia changanuzi. Hata hivyo, Showalter anasisitiza kwamba, licha ya tofauti za kijiografia, mikondo hii hujaribu kumwokoa mwanamke anayekuchukuliwa kama 'Wingine' (The other).

Ufeministi wa Kimarekani umehusishwa na wahakiki kama Annette Kolodny, Sandra M. Gilbert na Susan Gubar ambao wameandika kazi kama vile *The Mad Woman in the Attic: The Woman Writer and the Nineteenth-Century Literary Imagination* (1979) Katika kazi hii, waandishi hawa wanasema kwamba, sauti ya mwanamume imekuwa ikitawala kwa muda mrefu kwa sababu wanaume wamethibiti shughuli ya uandishi na asasi za uchapishaji. Halikadhalika, kwa sababu ya kutawala uwanja wa utunzi wa fasihi,

wanaume wamebuni taswira za mwanamke jinsi wapendavyo katika matini za fasihi hiyo.

Gilbert na Gubar wanahoji kwamba, uwezo huo wa wanaume umezua "taharuki ya utunzi" miongoni mwa wanawake na hivyo basi kuwafanya waogope kutunga kazi za kifasihi. Wanaamini kwamba hali hii itawatenga wanawake na hatimaye kuwaangamiza. Gilbert na Gubar wanasema, suluhisho la tatizo hili ni kwamba, wanawake wanapaswa kukuza "sentensi ya mwanamke" itakayochochea uhuru wa uandishi. Aidha, sentensi ya mwanamke kwa mujibu wa wataalamu hawa itawapa uhuru wanawake kutokana na taswira dumifu kuwahusu ambazo zimetawala maandishi ya kifasihi. Mifano ya taswira wanayotoa ni pamoja na 'malaika' ambayo si ya kiuhalisia kumhusu mwanamke katika jamii. Blessler (khj) anasema:

> ".....Ni bayana kwamba iwapo wewe sio malaika, basi wewe ni shetani. Taswira dumifu za aina hii zinazobuniwa na wanaume kuhusu wanawake katika fasihi zinapasa kuwekwa wazi, kuchunguzwa iwapo wanawake wataafikia uhuru wa kifasihi."
>
> (Tafsiri Yangu)

Ufeministi wa Uingereza nao unabainisha kwamba, jinsi wanawake wanavyosawiriwa katika fasihi huathiri moja kwa moja jinsi jamii inavyowachukulia. Kwamba wanawake hawanyanyaswi na kukandamizwa tu katika fasihi bali pia katika mifumo ya kitamaduni

na kiuchumi ambayo huwafanya kuwa wategemezi. Wahakiki wanaoegemea mkondo huu wanasema kuwa lengo la uhakiki ni kuibadilisha jamii bali si kuihakiki tu.

Ufeministi wa Kiufaransa unahusishwa kwa ukuruba na saikolojia changanuzi (Psychoanalysis). Saikolojia changanuzi inahusishwa na Sigmund Freud aliyeamini kwamba zubu ni kiungo kinachoashiria mamlaka aliyo nayo mwanaume na hivyo basi kuwaona wanawake kuwa wanaume wasiokamilika. Sigmund Freud aliamini kwamba wanawake wote walimwonea wivu mwanamume kwa sababu ya mamlaka aliyo nayo ambayo yanaashiriwa na zubu (wivu wa zubu).

Tulivyosema awali katika sehemu hii ya nadharia ni kwamba, ufeministi ni mkusanyo wa mikabala mbalimbali. Baadhi ya mikabala mahususi ni pamoja na ufeministi wa kibidhaa, ufeministi wa kidhanaishi, ufeministi wa kiharakati, ufeministi wa kisoshalisti, ufeministi wa kiutamaduni, miongoni mwa mikabala mingine.

#### 1.8.2.2 Ufeministi wa Kiharakati

Ufeministi wa kiharakati hutambulishwa na misimamo kwamba wanawake wananyanyaswa na kukandamizwa na wanaume. Pili, mpangilio mzima wa uana wa jinsi watu na vitu vinavyoainishwa umepangwa kwenye misingi ya kiume na kike. Tatu, kuwa 'kike' ni tokeo la miundo ya kijamii bali sio tofauti ya jinsia mbili tofauti.

Mkabala wa uana unaafiki utafiti wetu kwa sababu mada yetu inashughulikia masuala ya uana na jinsia hasa katika uchunguzi wa jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza

katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Aidha, katika kuegemea mkabala wa ufeministi wa kiharakati katika utafiti huu, tunatumainia kuchanganua matini ya kazi tulizozichagua kubainisha jinsi taswira dumifu za uana zinavyodhihirika kwa kuzingatia mpangilio wa kijamii wa majukumu ya wahusika kulingana na jinsia zao. Vilevile, tunatumia kigezo cha mkabala wa ufeministi wa kiuharakati kwamba 'kike' ni tokeo la miundo ya kijamii bali sio tofauti ya jinsia mbili tofauti katika kutathmini iwapo majukumu waliyotengewa wahusika katika vitabu tunavyovishughulikia kwa misingi ya jinsia hayawezi kubadilishanwa.

**1.8.2.3 Chukulizi za Kimsingi za Ufeministi**

Kwa jumla, vipengele au chukulizi za kimsingi za ufeministi ni pamoja na:

(i) Jamii ambayo imetawaliwa na mwanamume – inayoongozwa na itikadi ya kibabedume imerithishwa turathi na thamani fulani kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuishia kuwa chanzo cha kudumu kwa mfumo huu katika jamii kwa kipindi kirefu. Kwa kuendeleza fikra hizi (za unyonge wa), jamii inaishia kuakisi mawazo kama ya Aristotle aliyesema, 'kiumbe wa kike yuko alivyo kutokana na upungufu fulani' pamoja na St. Thomas Aquinas aliyesema kwamba wanawake ni wanaume wasiokamilika.

(ii) Kwa kukubali itikadi na fikra kuwa manamke ni mnyonge, tamaduni zinamsawiri mwanamke kama kiumbe duni na huendeleza mawazo haya katika sawia mbalimbali za jamii na kwa njia hiyo kuidhinisha udalilishaji wa wanawake.

(iii) Wanaufeministi wangependa kuona jamii ikitambua makosa ya mkabala huu au itikadi ya ubabedume. Hali hii inaakisiwa na fasihi na sanaa katika jamii ambayo inamsawiri mwanamke kwa kutumia taswira maalum na funge kama 'malaika', 'kahaba', 'mlezi', 'mhudumu wa baa', 'mke wa nyumbani', 'asiyetumia akili', 'mng'ang'anizi', 'chanzo cha maanguko' n.k. Wanawake wanapaswa kujikomboa kutoka kwa usawiri huu hasi na kujieleza wenyewe kwa njia chanya.

(iv) Ili kuweza kujikomboa kutokana na hali hasi au mfumo unaokandamiza 'wanawake' (sio lazima kila mfeministi awe mwanamke), wanapaswa kuzichanganua kazi za kifasihi zinazothaminiwa kama kazi muhimu na kuonyesha jinsi taswira duni zinavyochangia katika kuendeleza utamaduni wa kukandamiza. Wanawake wanapaswa kupambana na ubabedume kuihusu jinsia yao

(v) Huwazia upya sehemu inayounda kazi kuu katika fasihi, kutathmini uzoefu au tajriba ya wanawake na jinsi inavyotokeza katika maandishi ya kifasihi na kuuchunguza usawiri na uwasilishaji mzima wa wahusika wa kike katika kazi za fasihi ambazo zimeandikwa na wanawake.

(vi) Hudadisi na kushambulia uwasilishaji wa mwanamke kama 'Wingine' na huibua maswala na mijadala kama tofauti kati ya wanawake na wanaume ni suala la kibiolojia au linahusishwa na miundo ya kijamii.

(vii) Huchunguza na kuonyesha mahusiano ya kimadaraka au satua yaliyoko katika maandishi na maisha halisi kwa nia ya kuyabadilisha au kuyageuza, kuchukua tendo la usomaji kama tukio la kisiasa na kuonyesha jinsi mfumo wa ubabedume ulivyosaki katika jamii pamoja na matokeo yake

(viii) Kwamba harakati za wanamke za kujivumbua na kujitambua wao ni nani, kujielezea katika ulimwengu huu ndio msingi mkuu wa ukombozi sio tu kama viumbe binafsi, bali pia jamii nzima.

(ix) Huchunguza na kubainisha kama kuna lugha ya kiuandishi ambayo inaweza kuhusishwa na wanawake; na iwapo lugha hiyo ipo pia kwa wanaume; kama wanaweza kuionyesha au kuiakisi katika uandishi wao wa kiubunifu.

#### 1.8.2.4 Njia za Utekelezwaji

Ili kuchanganua kazi za fasihi ya Kiswahili ya watoto ambazo tumechagua kwa minajili ya utafiti huu kwa kutumia mikabala ya uana na ufeministi wa kiharakati, tumejiuliza maswali ya kijumla yafuatayo:

(i) Je, mwandishi ni wa kike au wa kiume? Katika kujiuliza swali hili tumelazimika kugawa matini tunazozihakiki kubainisha taswira dumifu za

uana katika makundi mawili: matini zilizoandikwa na waandishi wa kiume (androtexts) na matini zilizoandikwa na waandishi wa kike (gynotexts).

(ii) Wahusika wa kike na wa kiume wana majukumu na utendaji (action) gani kwenye matini? Swali hili limetuongoza kubaini tofauti za kiusawiri za wahusika wa kike na wa kiume katika kazi tunazozihakiki.

(iii) Wahusika wa kike wamepewa nafasi gani – ni wahusika wakuu au ni wahusika wajenzi?

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

(iv) Je, kuna taswira dumifu zozote za uana zinazojitokeza kuhusu wahusika wa jinsia zote kwenye kazi husika? Swali hili limetuongoza katika kubaini jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza kwa kuangalia vifaa vya kuchezea baina ya wahusika wa kike na wa kiume katika matini tunazozichunguza, masomo yao shuleni, taaluma za wahusika wa jinsia ya kike na ya kiume, sifa zao n.k.

(v) Wahusika wa kiume wana mielekeo ipi kuhusu wahusika wa kike?

(vi) Wahusika wa kike wana mielekeo ipi kuhusu wahusika wa kiume?

(vii) Miongoni mwa wahusika wa kike na wa kiume, ni nani anayemsaidia mwenzake na ni msaada wa aina gani?

(viii) Ni mhusika wa jinsia gani mwenye mamlaka?

Katika sura ya pili, tunajadili maswala ya kijumla ya utafiti huu ili kujiwekea usuli wa kutuwezesha kuchanganua data katika sura ya tatu na ya nne. Maswala hayo ni pamoja na fasihi ya watoto, sifa na majukumu yake, dhana 'jinsia' na 'uana' na taswira dumifu.

**Tanbihi**

1. Momanyi, C amejadili kwa kina jinsi mkabala wa asasi ya dini umetumiwa kutoa taswiraa potovu kumhusu mwanamke katika makala yake 'Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Fasihi ya Kiswahili Baada ya 2000: Kuyumbisha Uhalisi' katika *Kiswahili 2000*, p 23 –31.

# SURA YA PILI

## FASIHI YA WATOTO NA MAJUKUMU YAKE, UANA, JINSIA NA TASWIRA DUMIFU

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inajadili kwa ufupi maswala ambayo utafiti huu unayashughulikia. Lengo la hatua hii ni kuweka msingi utakaotusaidia kuchanganua data za matini ya fasihi ya watoto kubaini jinsi taswira dumifu za uana zinavyodhihirika katika kazi hizo. Vipengele tunavyoviangazia ni pamoja na fasihi ya watoto, majukumu ya fasihi hiyo, jinsia[1] uana[2]na taswira dumifu.

### 2.2 Fasihi ya Watoto na Sifa Zake

Fasihi ya watoto ni utanzu wa fasihi ambao hadhira yake kimsingi ni watoto. Juhudi za kubainisha sifa za fasihi hii zimepelekea kuibuka kwa vigezo vya kijumla ambavyo wataalamu wa fasihi ya watoto huegemea katika uainishaji wa kazi fulani kuwa ni fasihi au si fasihi ya watoto. Kwa hivyo, hakuna kigezo kimoja kinachotosheleza shughuli ya uainishaji wa sifa za fasihi ya watoto (Hunt 1991, Lesnik-Oberstein 1996, Huck 2001. Nodelman na Reimer (2003) waligundua kwamba, kuna machukulio ambayo watu wazima huwa nayo kuhusu utanzu wa fasihi ya watoto. Nodelman na mwenzake wanasema kwamba watoto hupenda hadithi kuhusu tajriba za utoto na kwamba hawana raghba ya kusoma na uwezo wa kuelewa tajriba ya watu wazima. Hatukubaliani na kauli hii kwa sababu watunzi wa fasihi ya watoto ni watu wazima na haiyumkiniki kutunga

fasihi isiyoakisi tajriba zao kama watu wazima. Kwa hivyo, mumo kwa mumo katika fasihi ya watoto inayoandikwa na watu wazima, mna tajriba za waandishi hao. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa hadithi za watoto hazipaswi kuelezea tabia au hali isiyokubalika kama vile ghasia, ujeuri, maadili yaliyozorota ambavyo vinaweza kuigwa na watoto. Kadhalika, wanasema kuwa hadithi za watoto hazipaswi kuwa na mambo yanayoweza kuwaogofya bali zinapaswa kuwa na mifano mizuri ya wahusika wanaopaswa kuigwa na ambao hutuzwa kwa sababu ya mienendo yao mizuri. Tunakubaliana na kauli hii ingawa fasihi ya aina hiyo haiakisi hali halisi katika jamii tunamoishi. Licha ya machukulio haya, kuna sifa za kijumla za fasihi ya watoto ambazo yaelekea zinakubalika ulimwenguni kote. Sifa hizi ni pamoja na:

(i) Huandikwa (hasa na watu wazima) kwa lengo la kusomwa na hadhira ya watoto na huhusu utoto.

(ii) Huwa na wahusika ambao aghalabu wengi huwa ni watoto. Hata hivyo, baadhi ya vitabu vya fasihi ya watoto huwa ni wahusika ambao ni watu wazima, wanyama, mazimwi na kadhalika. Kuhusu swala hili la uhusika katika fasihi ya watoto, May (1993:19) anasema kwamba ingawa waandishi wa fasihi ya watoto wanaandika kazi zao bila kuwa na habari kuhusu umri wa hadhira yao, hutumia wahusika wa kiuhalisia ili kuwavutia wasomaji chipukizi wa hadithi zao. Kauli hii ni kweli kwa sababu baadhi ya kazi za fasihi ya watoto huwa na wahusika ambao ni watu wazima.

(iii) Huwa sahili na hadithi huwa ya moja kwa moja.

(iv) Hadithi huwa fupi.

(v) Huandikwa kwa lugha na ploti sahili.

(vi) Hujishughulisha na maudhui ya kukua kwa watoto na hivyo basi huandikwa kwa mtazamo wa mtoto.

(vii) Huegemea mno fantasia.

(viii) Hujaribu kuwaelimisha watoto kuhusu masuala ya jamii, mienendo yao mbali na kuwa na hadithi za fantasia na usimulizi wa ugunduzi wa mambo mapya (adventure).

(ix) Mara nyingi hadithi huisha kwa furaha huku wema ukishamiri dhidi ya uovu. Aidha, fasihi ya watoto huandikwa kwa lengo la kutoa funzo fulani.

(x) Hutumia mbinu nyingine jenzi zaidi ya maandishi – michoro au picha.

## 2.3 Majukumu ya Fasihi ya Watoto

Swala la fasihi ya watoto huzua raghba kubwa miongoni mwa wanajamii. Hali hii huzuka kwa sababu fasihi hii huhusu kitengo cha jamii ambacho takriban kila mtu katika jamii ana uhusiano nacho. Aidha swala la fasihi ya watoto ni swala nyeti kwa sababu fasihi hii hutoa mchango mkubwa katika kukuza taswira wanayokuwa nayo watoto kujihusu wao wenyewe na ulimwengu pindi wanapokuwa watu wazima. Isitoshe taswira hii hubwiwa wakati wa utotoni. Ni fasihi hii ambayo kando na kukuza utamaduni wa Mwafrika na turathi za utamaduni huo, pia huwapa watoto maarifa na ukweli kuhusu hatua ya maendeleo iliyopigwa miongoni mwa jamii zao. Hellen Mwanzi (2006:49) anafumbata majukumu na umuhimu wa fasihi ya watoto wakati anaposema:

> "Kwa miaka na dahari, binadamu ametumia fasihi kukipokeza kizazi chipukizi maadili ya kuwasaidia kuishi na kufanikiwa.

> Kwa kuonwa kuwa mbegu ya kuendeleza kizazi cha baadaye, watoto wanapewa fursa ya kutangamana na vyanzo vya mtagusano katika jamii ili kujihisi kuwa katika jamii fulani. Hivyo basi, elementi ya mtagusano wa kijamii ni kipengele kimoja cha fasihi ya watoto inayoweza kubainika katika utanzu huu kote uliwenguni.[3]

Kutokana na kauli hii inabainika wazi kwamba fasihi ni nyezo muhimu ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira ya nyumbani kwao, jamii zao na ulimwengu kwa jumla. Hata kabla ya watoto kujua kusoma, jamaa zao, wanaowatunza na waalimu huwasomea hadithi kuhusu watu wa sehemu nyingine ulimwenguni na wakati mwingine hadithi za zamani kuhusu watu ambao maisha yao yanafanana na yao. Ujumbe katika hadithi hizi unaweza kuhifadhika katika kumbukumbu za watoto hawa maisha yao yote.

Fasihi ya watoto huchokoza fikra za watoto na kuwachochea kufikiria, huimarisha msamiati wao mbali na kuwasaidia kujifahamu kando na kuwafahamu watu wengine. Iwapo fasihi ya watoto inaakisi makundi kadha tofauti ya watu, fasihi hiyo itachangia mno katika kuwafanya watoto hao wajiheshimu na kuheshimu watu wa makundi hayo. Kwa hivyo, fasihi ya watoto inapasa kuwa 'kioo' ambacho kupitia kwayo watoto wanajiona, na pia dirisha la kuwawezesha kuutalii ulimwengu unaowazunguka. Fasihi ya watoto ina uwezo wa kuonyesha dhana kuwa watu tofauti wanaweza kufanya kazi pamoja bila ubaguzi wa aina yoyote.

Kwa bahati mbaya, sio kazi zote za fasihi ya watoto zinavyopitisha ujumbe kuhusu mambo ambayo jamii husika huwatarajia watoto wajifunze. Kazi nyingine aghalabu huwa na taswira dumifu za uana na ubaguzi wa namna moja au nyingine. Kwa kutojua kuwa baadhi ya taswira dumifu za uana zinawabagua, watazibwia. Tuliyosema kwingine katika tasnifu hii ni kwamba, awamu ya utoto ni awamu muhimu ya kukua ambapo bàadhi ya mambo ambayo mtu hujifunza hukongomelewa (fixated) na hujitokeza mtu anapokuwa mzima.

Kwa sababu watoto huvutiwa tu na ploti ya hadithi na wahusika, kuna uwezekano kwamba huenda wasijue kwamba kazi hizo zina ujumbe fulani unaowabagua kwa misingi ya jinsia au hata taswira dumifu za uana baguzi. Iwapo basi watoto wataruhusiwa waendelee kukumbana mara kwa mara na ubaguzi wa aina hiyo kupitia kwa maandishi kwenye vitabu vya fasihi yao pamoja na picha, kuna hatari kwamba upotovu huo utakuwa sehemu ya fikra zao, hasa ubaguzi huo unaposhadidiwa na ubaguzi katika jamii halisi wanapokuwa watu wazima. Hiki ndicho kiini cha uchunguzi huu ambao unabainisha wazi taswira dumifu baguzi za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

## 2.4 Fasiri ya Dhana 'Uana' na 'Jinsia'

Swala la uhusiano wa kiuana limekuwa mada ya mjadala miongoni mwa wataalamu mbalimbali wakiwemo wanaanthropolojia, wanaisimu, wanafasihi. Swala la lugha na uana limeshughulikiwa na wasomi wengi (Cameroon 1985, Coates 1986, Graddol & Swann 1989 na Simala 2000). Wataalamu wengi wanakubaliana kwamba uana ni swala la muundo wa jamii husika (social construct) na sio la kibiolojia. Swala la jinsia ndilo la

kimaumbile (Cameroon 1985, Coates 1986, Tuttle 1986, Graddol & Swann 1989 na Ostergaad 1992).

Tofauti za kijinsia ni swala la kibiolojia lakini jamii hutilia mkazo tofauti za kiuana. Kwa mujibu wa Strobel (1984) katika Hay na Stritcher (1984: 88) uana ni swala linalotokana na utamaduni lakini jinsia ni swala la kibiolojia. Mfano mzuri tunaoweza kuutumia kubainisha wazi tofauti ya dhana hizi mbili, 'uana' na 'jinsia' ni kwamba, mwanamume anapooa katika baadhi ya jamii za Kiafrika, huhitajika kulipa mahari kwa wazazi mwa msichana anayemwoa. Huu ni muunda wa jamii na hivyo basi ulipaji mahari ni swala la kiuana. Hata hivyo, katika ndoa hiyo, anayeshika mimba si mume bali ni mke aliyeolewa. Hili ni swala la jinsia au kimaumbile.

## 2.5 Swala la Uana Katika Mtazamo wa Kihistoria

Historia ya kale barani Afrika inadokeza habari muhimu kuhusu nafasi ya wanawake nyumbani na katika jamii. Jamii nyingi za Kiafrika ziliegemea ama mfumo wa kuukeni au kuumeni ambayo kupitia kwayo mwonoulimwengu wa familia ulipokezwa watoto

Katika jamii zilizoegemea kuukeni (matrilineal societies) mama alikuwa kiongozi wa familia na watoto walitambuliwa na kuhusishwa na wanawake waliowazaa. Pindi swala la umiliki wa mali lilipoanza kuzoeleka, hatua hiyo ilivuruga msingi wa mfumo wa uegemezi wa kuukeni na kusababisha mgawanyiko wa jamii katika makundi ya kijamii (social classes). Katika mwegemeo wa jamii kwenye mfumo wa kuumeni, watoto walitambuliwa na kuhusishwa na baba yao. Mwegemeo wa kuumeni ulianza kuzua

ukosefu wa usawa wa kiuana hasa swala la urithi wa mali lilipozingatiwa. Jamii zilizoegemea kuumeni ziliruhusu watoto wa kiume kurithi mali hasa ardhi na kuweka pembezoni watoto wa kike kuhusu swala hilo.

Mfumo wa mwegemeo wa kuumeni unadhihirika katika jamii nyingi ulimwenguni hivi sasa. Katika mfumo huu, inaaminika kwamba wanaume wako katika hadhi ya juu wanapolinganishwa na wanawake. Mfumo wa kuumeni ni mfumo bia na huchukua mielekeo mbalimbali kulingana na historia na tamaduni za jamii husika. Kadri na mapito ya wakati, wanawake walianza kupinga hatua ya kuwekwa pembezoni na wanaume. Dhana ya uana iliibuliwa na harakati za wanawake katika miaka ya 1970 kulalamika kwamba hatua ya kuwaweka pembezoni haikutokana na uasilia (nature), bali ina misingi yake katika jamii, tamaduni, siasa na historia. Kuhusu swala hili, Momanyi (2001: 54) anaandika:

> [...] kudunishwa kwa mwanamke hakutokani na udhaifu wa kimaumbile bali jinsi kiumbe huyu anavyochukuliwa kuwa duni katika utamaduni, hasa wa mfumo wa kuumeni. Hii humaanisha pia kuwa mtoto wa kike anapokua, hufanywa kuamini kwamba yeye ni kiumbe duni [...] Aidha itikadi za kuumeni zimethibitiwa katika maumbo tofauti ya kijamii na humuumba mwanamke katika hali ambazo zinaweza kutimiza matakwa ya mfumo huo wa kuumeni.[4]

## 2.6 Uana na Ugavi wa Majukumu

Jamii nyingi huegemea jinsia katika kugawa majukumu ya kikazi miongoni mwa watoto wa kike na kiume na wanawake na wanaume. Hata hivyo, majukumu ya kikazi yanayochukuliwa kuwa yanapaswa kutekelezwa na watu wa jinsia ya kike au jinsia ya kiume hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Tofauti kubwa za kijamii kati ya wavulana na wasichana na wanawake na wanaume zinatokana na mifumo iliyopo ya ugavi wa majukumu ya kikazi katika familia. Wasichana na wanawake hutekeleza majukumu mengi ya nyumbani kuliko wavulana na wanaume. Utafiti huu unabainisha jinsi hali hii inavyodhihirika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto kupitia kwa wahusika wa kazi tunazozihakiki.

## 2.7 Uana na Elimu

Mojawapo ya malengo ya serikali ya Kenya tangu uhuru ni kuwapa elimu sawa watoto wa jinsia ya kike na kiume. Kupitia elimu, mtu hujipatia maarifa muhimu ya kumwezesha kukabiliana na mazingira yake yanayozidi kubadilika kila uchao mbali na kujipatia ajira. Mbali na kuwa elimu ni muhimu, bado kuna ubaguzi mwingi wa kiuana katika vipengele vya mfumo wa elimu nchini Kenya. Haya yamebainika katika viwango vya elimu kati ya watoto wa jinsia ya kike na jinsia ya kiume. Idadi ya wasichana hupungua kadri mtu anapokwea ngazi ya elimu; huku katika eneo la taaluma, wanawake huwa wengi katika nyanja ya taaluma zisizokuwa na ushindani mkubwa katika soko la ajira.

Mafunzo wanayopewa watoto wa jinsia ya kike na kiume aghalabu hutofautiana. Mafunzo hayo mara nyingi hujikita kwenye nyanja zinazohusiana na maeneo ya majukumu ya kinyumbani. Watoto wa kike hupata mafunzo kwenye maeneo hayo tofauti na maeneo ya sayansi na teknolojia. Huku tukikubali kwamba ujuzi kazi za nyumbani ni muhimu, haupaswi kuwa eneo lililotengewa wanawake tu. Elimu na mafunzo vinapaswa kutolewa kwa usawa kwa watoto wavulana na wasichana ili waweze kushiriki ipasavyo kwenye uchumi kupita mipaka ya majukumu ya nyumbani. Uchunguzi huu unaangazia jinsi fafihi ya watoto inaweza kushadidia baadhi ya sera katika elimu.

Katika familia zisizokuwa na mapato ya kutosha, wazazi aghalabu huamua kuwaelimisha wavulana huku wasichana wakibaki nyumbani kufanya kazi za nyumbani. Kwa hivyo, elimu ya mtoto wa kike hutingwa na utamaduni ambao humtaka abaki nyumbani kuwalea ndugu zao wachanga, kupika, kuteka maji na kuni na kutekeleza usafi wa nyumbani.

## 2.8 Taswira Dumifu na jinsi Zinavyobainishwa

Hakuna rekodi yoyote ya ushahidi ulioandikwa kuhusu ni vipi, lini na wapi au ni chini ya masharti gani ambapo taswira dumifu za uana kuhusu majukumu ya jinsia ziliibuka au zilianza. Rekodi za historia zinaonyesha kwamba taswira dumifu za uana zilikuwepo na zilianza kuimarika katika himaya za kale za Ugiriki, Urumi, Misri na tamaduni nyinginezo katika sehemu hizo pamoja na tamaduni za Uchina, Japan na mataifa mengine ya Mashariki (Hurloch 1978:457)

Kulingana na Hurlock (Khj) makisio kuhusu chanzo cha taswira dumifu za uana yana misingi katika uchunguzi wa kianthropolojia na kisosholojia uliofanywa kuhusu ruwaza ya maisha ya asasi ya familia. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kwamba, uchunguzi wa rekodi za kimatibabu kuhusu tofauti za kimaumbile na kiakili (physiological) kati ya watu wa jinsia ya kike na kiume za karne nyingi zilizopita Kabla Masihi na kuhusu imani za kitamaduni unaweza kutoa mwanga kuhusu chanzo cha taswira dumifu.

Tangu utotoni, vifaa vya kuchezea pamoja na aina ya michezo ya watoto wa jinsia ya kike na kiume huwa tofauti. Kuna vinyago vinavyoidhinishwa na jamii kwamba vinafaa kuchezewa na wavulana na kuna vya wasichana pia. Tofauti hizi huendelezwa hadi utu uzimani kwa sababu ya kukongomelewa utotoni. Taswira dumifu za uana zinaweza kubainishwa kutokana na vifaa hivyo kwa sababu baadhi yavyo vimehusishwa na mamlaka na hadhi katika jamii husika.

Katika mwanda wa elimu, hata wakati watoto wa jinsia zote wanapata elimu katika shule sawa, masomo fulani huchukuliwa kuwafaa zaidi watoto wa jinsia fulani kuliko wa jinsia nyingine. Kwa mfano, wavulana wanahimizwa kutia bidii katika masomo ya sayansi na hisabati huku wasichana wakishajiishwa kujitahidi katika masomo kama vile Kiingereza, Kiswahili na sanaa nyingine.

Katika eneo la mihemko (emotions), inachukuliwa kwamba wasichana huwa na mihemko mno kushinda wavulana. Kwa mujibu wa taswira dumifu kuhusu wavulana, jamii inawatarajia wavulana kudhibiti mihemko yao kushinda wasichana. Inaaminika pia kwamba watu wa jinsia ya kiume huwa na mihemko mikubwa ya kukasirika na woga

huku watu wa jinsia ya kike wakitawaliwa taswira dumifu za mihemko ya furaha na upendo (affection).

Taswira dumifu za uana pia hubainika wazi katika sifa za bainifu za kibinafsi (personality traits) ambazo huchukuliwa kuwa faafu kwa watoto wa kike nyingine kwa watoto wa kiume. Kwa mfano, sifa bainifu za kibinafsi miongoni mwa watoto wa kike ni pamoja na utegemezi (dependency), kukaa tu (passivity) na watiifu. Halikadhalika, sifa bainifu za watoto wa kiume ni pamoja na viongozi katika mambo na shughuli mbalimbali (dorminant) wasiokuwa watulivu (aggressive). Akishadidia hoja hii, Palmer (1989:14) anaeleza:

> "Wanadharia kama Phylis Chesler, akiandika mwanzoni mwa miaka ya sabini anashadidia hali ya ukandamizwaji wa mwanamke na kuwasilisha kwa jumla mtazamo hasi nafasi yake. Chesler na wenzake walimnasibisha mwanamke na sifa kama vile kukaa tu, utegemezi na kutoweza kufanya maamuzi kivyao. Huku wanadharia hawa wakichukulia jinsia ya kiume kuwa ukawaida, walichukulia jinsia ya kike kuwa ni kasoro au 'taksiri ya kiakili."[5]
>
> (Tafsiri Yangu)

Vilevile kuna taaluma ambazo hunasibishwa na watu wa jinsia ya kiume huku nyingine zikichukuliwa na jamii kwamba zinafaa zaidi kushughulikiwa na wanawake. Hali hii pia imechochea kuimarika kwa taswira dumifu za uana. Tangu utotoni watoto hutiwa moyo na wakati mwingine kushinikizwa kujiandaa kwa taaluma zinazoingia kwenye kategoria

hii ya taswira dumifu. Wavulana kwa mfano wanatarajiwa kuwa viongozi katika sekta ya biashara na viwanda miongoni mwa taaluma nyingine. Iwapo wenzao wa kike wanaingia katika taaluma zinazochukuliwa na jamii kuwa himaya ya wanaume, wanatarajiwa kuwa wafanyakazi wa matao ya chini. Kwa hivyo, watoto wa kike wanashajiishwa na jamii kuingia katika taaluma zinazohusu 'kazi ya wanawake' – mathalan ualimu, uuguzi, kazi za nyumbani na taaluma nyingine ambapo kazi yao itachangia katika kuboresha maslahi ya wengine (Maccoby & Jacklin 1974, Shields 1975 na Whiting & Edwards 1973).

## 2.9 Hitimisho

Sura hii imejishughilisha na maswala ya kimsingi ya utafiti huu; fasihi ya watoto na sifa zake, majukumu ya fasihi ya watoto, fasili ya dhana za jinsia na uana na taswira dumifu. Imebainika kwamba fasihi ya watoto ni utanzu unaoandikwa na watu wazima huku wakilenga hadhira ya watoto. Miongoni mwa sifa zake za kimsingi ni kwamba hadithi za utanzu huu huwa sahili huku maudhui mengi yakilenga kukua kwa watoto. Kadhalika, imebainika kwamba fasihi ya watoto ina jukumu muhimu la kufanikisha mtagusano wa kijamii na kupokeza kizazi chipukizi maadili ya jamii.

Sura hii pia imebainisha kwamba jinsia ni maumbile ya kibaolojia ilihali uana ni muundo wa jamii. Kadhalika, sura hii imeangazia mawazo ambayo japo hayajathibitishwa kisayansi, yameathiri pakubwa na kuchochea kushamiri kwa taswira dumifu za uana katika jamii. Mawazo haya hasa yamejikita katika tofauti kati ya jinsia ya kike na kiume. Tofauti hizi kwa mujibu wa Hurlock (1978) ni pamoja na zile za kimaumbile, kifiziolojia, silika, tofauti za kiakili, tofauti za ufanisi, mihemko, tofauti za kiafya, tofauti ya kiwango

cha vifo na mafunzo ya vitabu vitakatifu hasa Biblia. Hatimaye sura hii imejadili mihimili mikuu ambayo kwayo tunaweza kuegemea ili kubaini taswira dumifu. Mihimili hii ni pamoja na vifaa vya kuchezea, masomo shuleni, mihemko, sifa bainifu za kibinafsi na taaluma.

Katika sura inayofuata tunahakiki fasihi ya Kiswahili ya watoto kubainisha jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza, kutathmini iwapo kuna uwakilishi sawa wa wahusika wa jinsia zote na kubaini iwapo kuna taswira dumifu baguzi katika kazi hizo.

## Tanbihi

1. Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI), istilahi 'uana' na 'jinsia' ni visawe. Lakini katika utafiti huu, dhana hizi zimetumika kwa maana tofauti na hiyo ya kileksika; kwamba 'jinsia' ni dhana inayorejelea maumbile ya kibiolojia kwa mfano kuwa mvulana au msichana. Kwa mfano, mwanamke kushika mimba na kuzaa ni hali ya maumbile (jinsia),

2. 'uana' ni istilahi inayotumiwa katika utafiti huu kwa maana ya muundo wa jamii. Kwa mfano mwanamume kutakiwa alipe mahari anapooa ni swala la uana.

3. Mwanzi, H.O. amejadili umuhimu wa fasihi ya watoto kwenye makala yake: 'Childen's Literature: The Concept of Socializing the Young' katika *The Nairobi Journal Of Literature* No. 4, Machi 2006, p 49-61 Taz. pia Cameroon, D. *Feminism and Linguistic Theory*. London: McMillan. 1985, p. 24

4. Rej. Makala ya Clara Momanyi, 'Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Fasihi ya Kiswahili Baada ya 2000: Kuyimbisha Uhalisi' katika *Kiswahili 2000*. Dar Es Salaam: TUKI, p 23 – 33.

5. Rej. Palmer, P, 'Feminity and its Constuction', katika *Contemporary Women's Fiction: Narrative practice and Feminist Theory*. New York: Harvester Wheatleaf, p 13 - 41

# SURA YA TATU

## 3.0 TASWIRA DUMIFU ZA UANA KATIKA *MSICHANA MLEMAVU NA NDUGU ZAKE, MWANASESERE WA MOSI* NA *MGOMBA CHANGARAWENI*

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia uchanganuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto vilivyoandikwa na waandishi wa kiume / matiniume[1] (androtexts) ili kubainisha ni kwa jinsi gani taswira dumifu za uana zinavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Vitabu hivyo ni: *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* (K.W. Wamitila, 2006), *Mwanasesere wa Mosi* (Demere Kitunga, 2002) na *Mgomba Changaraweni* (Ken Walibora, 2004)

Hali kadhalika sura hii inatathmini iwapo wahusika wa kike na kiume katika kazi hizi wamesawiriwa kwa usawa kwa misingi ya jinsia zao. Sura hii pia inachunguza iwapo waandishi wa kazi hizi wanawakilisha kwa idadi sawa wahusika wa jinsia ya kike na kiume katika kazi hizi. Sababu ya kuangazia kipengele hiki ni kwamba, wasomaji hujitambulisha na kujinasibisha na wahusika wa jinsia zao kwenye vitabu. Hivyo basi, ukosefu wa wahusika wa jinsia ya kike na kiume katika matini za vitabu vya fasihi ya watoto, kwa mfano, kunaweza kuwanyima fursa watoto wa kike na wa kiume kujinasibisha na jinsia yao na kutambua nafasi yao katika jamii. Aidha uhalisia uliopo katika jamii ni kwamba kuna watoto wa jinsia za kike na kiume na hivyo basi wanapoandika, waandishi wa fasihi ya watoto hulenga hadhira ya watoto wa jinsia zote na wala sio watoto wa jinsia moja.

### 3.2.0 *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*

### 3.2.1 Muhtasari wa *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*

*Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* ni mojawapo ya kazi za kifasihi za watoto zilizotungwa na K.W. Wamitila. Wamitila ni mmoja wa watunzi maarufu nchini Kenya ambaye amechangia karibu tanzu zote za fasihi mathalan riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi na utanzu wa fasihi ya watoto. Baadhi ya tungo zake ni riwaya za *Nguvu ya Sala* (1999) *Bina-Adamu* (2002) na *Msimu wa Vipepeo* (2007), tamthilia za *Wingu la Kupita*, *Pango* na *Sumu ya Bafe*, Tamthilia *ya Maisha*, (diwani ya mashairi aliyoihariri) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (mkusanyo wa hadithi fupi aliouhariri). Baadhi ya vitabu vya mwandishi huyu katika utanzu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto ni pamoja na *Yatima* (2006), *Zimwi la Leo* (2002), *Kadogo na Majini ya Nyanya* (2004) *Kuku na Mwewe* (2007) *Mwanakijiji na Miwani* (2007), *Kesi ya Kuchekesha* (2007) na *Jumba la Huzuni* (2007)

*Msichana Mlemavu na Ndugu zake* ni hadithi kumhusu Shijango na watoto wake watatu, Koki (msichana) na nduguze wawili wa kiume, Ngoa na Gele. Ngoa ndiye kifungua mimba, akifuatiwa na Gele huku Koki akiwa ndiye kitinda mimba. Mama yao alifariki mara tu baada ya kumzaa Koki.

Koki na nduguze wana hulka tofauti. Huku Koki akiwa mwerevu na anayependa kuwasaidia watu, nduguze ni watoto wanaopenda ubinafsi. Kwa sababu ya tabia yake nzuri, watu wengi walitamani Koki arithi mali ya baba yake. Lakini katika jamii hiyo, wasichana hawaruhusiwi kurithi mali. Mali inafaa kurithiwa na wavulana tu.

Maisha ya familia hiyo yanabadilika ghafla bin vuu Mzee Shijango anapopofuka. Wanatafutwa madaktari wa kila aina kumtibu Shijango lakini wanashindwa. Anatokea mwamba wa miti shamba - Mama Mongo ambaye anapendekeza kwamba dawa ya pekee inayoweza kumtibu Shijango inatokana na majani ya mvinde.[2]

Hali ya afya ya Shijango inapozorota, Ngoa anaomba sehemu yake ya urithi na kuondoka nyumbani kwenda kutafuta majani ya mvinde ili baba yao aweze kupona. Baada ya kupatiwa sehemu ya urathi wake, anaondoka nyumbani. Juhudi zake za kutafuta majani ya mvinde zinaambulia patupu. Akiwa kwenye shughuli za kusaka majani ya mvinde, anakutana na mwanamke mzee ajabu aliyeketi kando ya njia. Mama huyo ana taabu ya njaa na anamwomba Ngoa amsaidie lakini anakataa.

Hali ya afya ya Shijango inakuwa mbaya zaidi na mkono wake kufa ganzi. Inamlazimu mwanawe wa pili, Gele naye aondoke nyumbani kwenda kutafuta dawa ya kumtibu baba yao. Aidha Gele anaondoka baada ya kupewa sehemu ya urithi wake. Juhudi zake za kutafuta majani ya mvinde pia hazifui dafu. Anapokutana na yule kikongwe mkata, naye pia anakataa kata kata kumsaidia – ingawa ana uwezo wa kufanya hivyo.

Hali ya Mzee Shijango inapokuwa si hali tena, Koki analazimika pia kuondoka nyumbani kwa punda kwa sababu amelemaa mguu mmoja. Juhudi zake za kutafuta majani ya mvinde hazifanikiwi kamwe hadi anapokutana na yule ajuza maskini. Tofauti na nduguze waliompa kisogo maskini huyo, Koki anamgawia chakula alichobeba ili kimfae akiwa safarini. Jambo ambalo hawakujua kaka zake ni kwamba ajuza huyo ndiye aliyefahamu

yalikopatikana majani ya mvinde. Kama ishara ya shukrani kwa Koki ambaye anamuauni kutokana na njaa, anamwelekeza yanakopatikana majani ya mvinde.

Baada ya kuyapata majani ya mvinde, Koki anakutana na nduguze, Ngoa na Gele ambao kwa wivu wanampokonya yale majani na kumpiga dada yao mpaka anazirai. Wanarudi nyumbani na kumtengenezea baba yao dawa kutokana na majani hayo ambayo inamponya Shijango. Wanapoulizwa ikiwa walimwona Koki, wanadanganya kuwa hawakuwahi kumwona. Hali hii inamhuzunisha sana Shijango.

Siku moja pale kijijini anafika mtu kutoka pwani na kuwaeleza wanakijiji kisa cha ajabu kuhusu mfugaji aliyesikia maua yakiimba. Shijango anapata habari kuhusu kisa hicho na kuamua kukifuatilia. Anazuru sehemu iliyoelezwa kutokea kisa hicho na kwa bahati nzuri anakutana na yule mfugaji aliyezua kisa hicho. Wakiwa kwenye majadiliano, wanasikia sauti nyuma ya maua. Shijango anajitoma kwenye kichaka kwa nguvu zote na kumkuta Koki kwenye pango lililokuwa mahala hapo. Anamchukua na kumbeba begani na kumpeleka nyumbani.

Koki anaeleza ukweli wa mambo kuhusu alivyodhulimiwa na ndugu zake na kunyang'anywa majani ya mvinde. Ngoa na Gele wanajaribu kutoroka. Mzee Shijango anapiga ripoti katika kituo cha polisi kuhusu wanawe hao (wa kiume) waliomtendea binti yake uhalifu mkubwa kama ule. Wanasakwa kwa muda mrefu na kutiwa mbaroni na hatimaye kufungwa.

### 3.2.2 Taswira Dumifu za Uana Katika *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*

Katika sura ya kwanza, tumesema kwamba uchanganuzi wa kazi ya kifasihi kwa kuegemea mkabala wa uana na ufeministi humuhitaji mhakiki kujiuliza maswali yafuatayo ya kijumla: Je, mwandishi wa matini inayoshughulikiwa ni wa kike au ni wa kiume? Pili, wahusika wa kike na wa kiume wana majukumu na shughuli au utendaji (action) gani kwenye matini. Tatu, wahusika wa kike wamepewa nafasi gani kwenye matini husika – ni wahusika wakuu au ni wahusika wajenzi? Je, kuna taswira dumifu zozote za uana zinazojitokeza kuhusu wahusika wa jinsia zote katika kazi huzika? Tano, wahusika wa kiume wana mielekeo ipi kuhusu wahusika wa kike? Sita, miongoni mwa wahusika wa kike na kiume, ni nani anayemsaidia mwenzake na ni msaada wa aina gani? Na mwisho, ni mhusika gani mwenye mamlaka. Maswali haya yanatusaidia katika ubainishaji wa taswira dumifu za uana katika kazi tunazozishughulikia.

Taswira dumifu ya uana inayojitokeza mwanzoni mwa hadithi hii ni kuhusu urithi wa mali. Utamaduni ambamo kazi hii imeibuka hauwaruhusu wanawake kurithi mali kutoka kwa baba zao. Wanaokubaliwa kurithi mali hiyo ni watoto wa kiume. Kwa hivyo, ingawa Koki ni mwerevu, mwenye utu unaompelekea kupenda kuwasaidia watu wengine, hawezi kurithi mali ya baba yake anayempenda kwa sababu ya taswira dumifu ya uana iliyotokana na muundo wa jamii – kwamba mtoto wa jinsia ya kike hawezi kamwe kurithi mali. Mwandishi anadokeza haya anaposema:

> Watu wengi walitamani Koki airithi mali ya baba yake. Lakini wote walijua jambo moja. Katika jamii yao, ilikuwa vigumu kwa msichana kuirithi mali ya babake. Katika kabila lao siku hizo, waliorithi mali walikuwa wavulana tu. [....] Watu walijua kuwa Ngoa alikuwa mtu wa kujipenda. Gele naye hakumfikiria mtu mwingine. Koki tu ndiye aliyekuwa na roho nzuri. 'Koki akiirithi mali ya babake atatusaidia,' walisema kila wakati (uk. 2-3)
>
> (Msisitizo Wangu)

Akiangazia swala la urithi wa mali miongoni mwa jamii zenye tamaduni tofauti nchini Kenya baada ya kutathmini mivutano inayotokana na jamii ama kwa kuegemea kuumeni au kuukeni, Njogu Waita (1997) anakubali kwamba kwa jumla, utamaduni umebakia kuwa kikwazo cha kiitikadi kinachopelekea watoto wa kiume kuendelea kupendelewa katika urithi na umiliki wa ardhi. Hali hii pia inajitokeza katika kazi ya fasihi ya watoto tunayoihakiki. Kumpendelea mtoto wa kiume na kumweka pembezoni mtoto wa kike kwa misingi ya urithi wa mali ni kuendeleza taswira dumifu za uana.

Kadhalika, katika kumsawiri Koki kuwa kilema, mwandishi anaibua taswira ya upungufu au udhaifu ambao jamii ambamo kazi hii imeibuka inamchukulia mtoto wa kike kuwa nao. Hata hivyo tunabaini kwamba mwandishi anajaribu kimaksudi kumwepusha mtoto wa kike na taswira hii dumifu ya uana iliyojikita katika jamii kuhusu urithi wa mali kwa kutamatisha hadithi hii kwa mdokezo kwamba, hatimaye Koki alirithi mali ya baba yake.

Swala kuhusu haki ya urithi wa mali kati ya watoto wa jinsia ya kike na kiume nchini Kenya ni swala la mjadala. Mjadala huu unatokana na msingi kwamba taswira dumifu ya uana katika suala hilo imesakini katika jamii. Kumekuwepo na juhudi za kimaksudi nchini Kenya kukabiliana na taswira hiyo dumifu baguzi hasa katika kielelezo cha katiba mpya iliyopendekezwa. Rasimu hii ya katiba inasema hivi kuhusu kipengele cha uana na hasa kuhusu urithi wa mali:

> Wanawake na wanaume wana haki ya usawa katika nafasi za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii [...] Wanawake na wamaume wana haki sawa ya urithi wa mali [...] kwamba sheria, tamaduni au itikadi zoyote zinazohujumu maslahi na hadhi ya wanawake au wanaume haziruhusiwi.*
>
> (Tafsiri na Msisitizo Wangu)

### 3.2.3 Wahusika, Hulka na Majukumu Yao

#### 3.2.3.1 Wahusika na Hulka Zao

Mhusika mkuu katika hadithi ya *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* ni Koki ambaye ni mhusika wa kike. Wahusika wengine ni pamoja na Ngoa, Gele, baba yao Mzee Shijango, Mama Mongo ambaye ni mganga, mwanamke mzee na mfugaji mifugo. Katika hadithi hii mwandishi amewasawiri wahusika hawa kwa njia tofauti kwa lengo la kufanikisha maudhui yake.

---

*Kenya Gazette Supplement, 2005, *Katiba Mpya Iliyopendekezwa,* Uk 30

Koki amesawiriwa kama mhusika mkarimu, mnyenyekevu na asiyependa ubinafsi. Tofauti na ndugu zake wa kiume wanaodai sehemu ya urithi kutoka kwa baba yao kabla ya kuondoka kwenda kutafuta dawa ya majani na mvinde ili kuyaokoa maisha ya baba yao, Koki hafanyi hivyo. Kitu cha pekee ambacho Koki anamwomba baba yake ni punda wa kusafiria kwa sababu ya mguu wake mbovu.

Taswira dumifu ya uana kuhusu ulezi inajitokeza kupitia kwa Koki ambaye daima alikuwa karibu na baba yake aliyeugua. Ngoa aliutumia muda wake mwingi kujinadhifisha mbele ya kioo. Mwandishi amemsawiri mtoto wa kike kama mlezi wa baba. Aidha, hatua ya Koki kumpatia chakula mwanamke mzee katika hadithi hii ni hatua ya kimalezi. Mwandishi anadokeza haya ifuatavyo:

> Wakati huu Ngoa alikuwa anajiangalia kwenye kioo chake chumbani. Lakini aliweza kuyasikia maneno ya Mama Mongo. Gele naye alikuwa bado anacheza na mishale yake. Naye pia aliyasikia maneno hayo. Koki kama kawaida yake, alikuwa karibu na baba yake. Alikuwa ameushika mkono wa kulia wa babake. (Uk. 3)
>
> (Msisitizo Wangu)

Katika hadithi ya *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*, Koki ndiye aliyefanikiwa kupata dawa ya majani ya mvinde ambayo ingetumika kumtibu baba yao, Mzee Shijango. Hata hivyo, hadithi inachukua mkondo tofauti pale ambapo ndugu zake wa kiume, Gele na

Ngoa (ambao majina yao yanawakilisha wivu) wanampokonya dawa hiyo kwa sababu ya kuwa na nguvu kumshinda. Kwa sababu ya udhaifu wake unaotokana na ulemavu wa mguu wake wa kushoto, Koki anashindwa kuitetea haki yake. Kisa hiki ni ishara ya taswira dumifu ya uana katika jamii pana ambayo inamwona mwanamke au mtoto wa kike kama kiumbe dhaifu – asiyekuwa na uwezo wowote mbele ya mwenzake wa kiume na hivyo basi asiyeweza kutetea haki yake. Kisa hiki kinadhihirisha kwamba wahusika wa kiume katika matini hii wana mielekeo hasi dhidi ya mhusika wa kike. Kwa sababu ya kuwa na nguvu kumshinda, wanatumia nguvu hizo kumdhulumu.

Kadhalika, baada ya Koki kudhulumiwa na kaka zake, anabaki akihangaika msituni hadi mfugaji mifugo (mwanaume) anaposikia wimbo wa 'maua yanayoimba'. Shijango anafunga safari hadi mahala hapo na kumuokoa Koki aliyekuwa pangoni. Tunaambiwa:

> Shijango hakusubiri sauti inyamaze mara hii. Alijitoma kwenye kichaka hicho kwa nguvu zote. Alimkuta Koki kwenye pango lililokuwa hapo. Kando yake palikuwa na masega ya asali ya nyuki. Alimchukua na kumweka kwenye mabega yake. Safari ya kurudi nyumbani ilianza tena.... (Uk. 19)

Dondoo hili linashadidia taswira dumifu na imani iliyojikita katika jamii kwamba watu wa jinsia ya kike daima ni wategemezi wa watu wa jinsia ya kiume. Kwa hivyo, Koki hangeweza kamwe kufanikiwa bila usaidizi wa baba yake ambaye ni kiwakilishi cha pote la jinsia ya kiume. Ni kinaya kikubwa kwenye hadithi hii kwamba katika hadithi hii

ambapo nduguze Koki wanastahili kumtunza dada yao kwa sababu ya kuwa mlemavu na dhaifu, wanatumia fursa hiyo kumdhulumu kwa sababu ya kumwona kuwa tisho kuu katika urithi wa mali ya baba yao.

### 3.2.3.2 Majukumu ya Wahusika

Katika kuangazia misingi ya kiutamaduni ya kutofautisha majukumu ya uana, mahusiano ya mamlaka na udhibiti wa raslimali miongoni mwa jamii ya Waluo, Benjamin M. Odhoji (1977) anadokeza:

> Watoto wanahesabiwa kuwa wa mwanamume ingawa maumbile ya kibaolojia kama vile kutunga mimba, kujifungua na kunyonyesha humwezesha mwanamke humpa fursa ya kujishughulisha na kutoa mafunzo kwa mtoto kulingana na matakwa ya jamii kutegemea jinsia ya mtoto huyo. Hivyo basi, watoto wa jinsia ya kike huandaliwa kujishughulisha na ukusanyaji vyakula wanapokuwa watu wazima huku wavulana wakijishughulisha na kuchunga mifugo, usasi na kuwalinda dada zao wasidhuriwe na maadui. Majukumu haya yote huwaandaa wavulana kutekeleza majukumu sawa na hayo wanapokuwa watu wazima.[3]
>
> (Tafsiri Yangu)

Katika *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*, wahusika wamepewa majukumu ya kiutendaji kuzingatia jinsia yao. Koki kama tulivyodokeza awali katika sura hii amenasibishwa na taswira dumifu ya ulezi. Ndugu zake, wamesawiriwa kama wawindaji kwa sababu wana nyuta na mishale. Mwandishi anadokeza:

> Gele alifanana kwa kiasi kikubwa na Ngoa [....] Alisema kuwa alikuwa shujaa na bingwa mkubwa wa kuitumia mishale. Gele aliupitisha wakati wake mwingi akijizoeza jinsi ya kutumia mishale na uta. Mara nyingine alienda kwenye msitu uliokuwa hapo karibu kuwaua ndege. Wakati mwingine alichukua manati yake na kwenda kuwinda bundi kwenye mapango yaliyokuwa huko chini. Kama alivyokuwa Ngoa, Gele pia hakumfikiria mtu mwingine. Koki kwa upande wake, alikuwa tofauti kabisa [...] Koki alikuwa mwerevu na alipenda kuwasaidia watu sana. Babake alimpenda sana. (Uk.1&2)

Aidha, pinde na mishale aliyo nayo Gele, kwenye hadithi hii ni vifaa vinavyoashiria mamlaka. Isitoshe shughuli za kuwinda msituni anazozifanya mhusika huyu zinaashiria nguvu za kimwili. Kwa hivyo, mhusika wa kiume katika kazi hii amekwezwa hadhi kwa kusawiriwa kama shujaa huku picha ya mhusika wa kike ambayo inajitokeza ikiwa ni ya mtu mnyonge, mlemavu na ambaye kamwe hawezi kujitetea.

Akitoa hoja kuhusu usawiri wa mtoto wa kike na mwanamke kwa jumla katika fasihi, Momanyi (2001) anadai kwamba waandishi hawana budi kuumba wahusika wa kike kwa kuwakuza ili waweze kuvuka mipaka ya jinsia na kuwa vielelezo halisi vya binadamu wanaoweza kujisimamia wenyewe. Kwamba wahusika hao wakuzwe kimawazo ili kuwapa nafasi wanayostahili katika nyaraka za historia. Tunakubaliana na maoni ya Momanyi hasa kwa kuzingatia utanzu wa fasihi ya watoto. Waandishi wa fasihi hii wanapaswa kuwasawiri wahusika wa kike wakiwa katika mapambano dhidi ya mikatale ya kitamaduni idhalilishayo.

#### 3.2.3.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume

Mwandishi wa *Msichana Mlemavu Na Ndugu Zake* ametumia idadi sawa ya wahusika wa kike na wa kiume. Wahusika wa kike ni pamoja na Koki ambaye ni mhusika mkuu, mama yake Koki na nduguze (ambaye anatajwa tu kwenye hadithi) Mama Mongo (mwamba wa mitishamba), na mwanamke mzee ajabu. Wahusika wa kiume ni pamoja na Ngoa na Gele, Mzee Sijango na mfugaji.

## 3.3 *Mwanasesere wa Mosi*

### *3.3.1* Muhtasari wa *Mwanasesere wa Mosi*

Demere Kitunga ni mwandishi anayeinukia wa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Mtafiti huyu hana habari kuhusu kazi nyingine iliyotungwa na mwandishi huyu isipokuwa *Mwanasesere wa Mosi*.

*Mwanasesere wa Mosi* ni hadithi kumhusu Mosi, msichana mwenye umri wa miaka sita ambaye anatamani mwanasesere. Mama yake anaahidi kumzawadia mwanasesere wa kipekee. Mosi hajui atakavyokuwa mwanasesere huyo hadi mama yake anapomzawadia Kida, mwanasesere anayemsaidia kujitambua. Hata hivyo, safari ya kumpata Kida ni ndefu na ya kukatisha tamaa. Siku zote Mosi amekuwa akitamani kuwa na mwanasesere wake mwenyewe. Rafiki zake wote ambao pia ni majirani – Namsi na Kunda wana wanasesere. Wakati mwingine Mosi ananyimwa mwanasesere na dada yake Kunda wakati anapomhitaji zaidi ili amchezee. Anahuzunika sana na kuwaza kwamba laiti angalikuwa na mwanasesere wake asingalidhulumiwa hivyo. Mwishowe mama ya Mosi anatimiza ahadi yake kwa kumnunulia mwanasesere wa kipekee.

Kitabu hiki kina takriban sifa zote za vitabu vya fasihi ya watoto tulizoorodhesha katika sura ya pili. Ploti na hadithi yenyewe ni sahili. Wahusika ni watoto, imeandikwa kwa lugha sahili na imeishia kwa furaha kwa sababu ndoto ya Mosi ya kumiliki mwanasesere wake binafsi inatimia. Vilevile sehemu kubwa ya kitabu hiki imechukuliwa na picha au michoro inayomsaidia mtoto katika kuielewa hadithi. Hata hivyo utafiti huu haujishughulishi kamwe na uchunguzi wa michoro kwa sababu michoro hiyo huwa si kazi ya mwandishi.

### *3.3.2* Taswira Dumifu za Uana katika *Mwanasesere wa Mosi*

Fahiwa ya kimsingi tunayopata kutoka kwa anwani ya kitabu hiki – 'Mwanasesere wa Mosi' ni ile ya kusawiriwa kwa mtoto wa kike kama mlezi wa jamii. Aidha taswira dumifu za uana zinazojitokeza katika kazi hii ni kwamba jamii huwakuza watoto kwa

kuwatengea majukumu kutegemea na jinsia yao. Mosi, Kunda na Namsi ni viwakilishi tu vya jinsi jamii pana huwalea watoto katika mazingira ya kuwaandaa kuwa walezi pindi watakapokuwa watu wazima. Vifaa vya kuchezea ambavyo watoto wa kike wanatengewa na jamii ni wanasesere au watoto wa bandia ambao kwa sababu ya utoto wao, wanaamini kabisa kuwa ni watoto wa kweli wanaohitaji malezi mema. Isitoshe, michezo mingi wanayocheza inaakisi nafasi ya mwanamke katika jamii. Tunasoma kwenye hadithi:

> Mosi, Kunda na Namsi ni majirani. Wanasoma darasa moja. Mara kwa mara, wanapenda kucheza pamoja. Wanacheza kombolela, kimamamama[3], rede na michezo mingine mingi. Lakini mara nyingi wanapenda kuchezea mwanasesere.Wanageza kuwa mama, wanapocheza kimama mama, mmoja anakuwa mama mgeni. Mwanasesere wa Kunda anakuwa mtoto na wa Namsi dada yake. (Uk.2)
>
> (Msisitizo Wangu)

Taswira dumifu ya uana kuhusu mahala pa mwanamke na majukumu yake ya ulezi kulingana na jamii nyingi za Kiafrika pia imetiliwa nguvu zaidi na michezo ya kitoto ya akina Mosi na Kunda. Tunaambiwa:

[....] walimbeba 'mtoto' wakampikia chakula, wakamlisha, wakambadilisha nepi, wakambembeleza alale, wakamtandikia kitanda na kumlaza. (Uk.9)

(Msisitizo Wangu)

Dondoo hili linatudokezea kwamba utamaduni ambamo kazi hii imeibuka umemtengea mwanamke mahala pake maalum ambapo ni jikoni na kwamba mahala hapo ni karakana yake ya kuipikia na kuilisha jamii. Hali kadhalika jamii humtarajia mwamamke kuhakikisha kwamba maslahi ya kimsingi ya jamii yake kama vile kuitandikia vitanda na kuistarehesha yanatimizwa.

Taswira nyingine dumifu ya uana inayojitokeza katika *Mwanasesere wa Mosi* ni ile ya kutofautisha vifaa vya kuchezea vya watoto wa jinsia ya kike na kiume. Ingawa mwandishi ametumia wahusika wengi wa kike katika kazi hii, anapenyeza sauti na mtazamo wa mwanamme kuhusu vifaa wanavyotumia kuchezea watoto wa kiume kupitia kwa baba yake Mosi. Mosi aliponyimwa mwanasesere wa Kunda na dada yake Kunda, alirudi nyumbani akiwa amenuna. Baba yake alimfariji na kumshauri:

> "Sisi tulipokuwa watoto tulitengeneza wenyewe vitu vya kuchezea. Tena vizuri kuliko haya maplastiki ya dukani. Tuliweza kutengeneza magari, baiskeli na hata eropleni kwa mabua. Siku hizi ninyi mnaona kuwa kila kitu lazima kinunuliwe dukani...." (Uk.5)

(Msisitizo Wangu)

Vifaa vya kuchezea vya watoto wa kiume ni vifaa vinavyohusishwa na nguvu na mamlaka. Kwa mfano, gari ni chombo kinachohusishwa na fahari na ukwasi katika jamii zetu. Kwa hivyo, hatukosei kudai kwamba, kuna uwezo mkubwa wa kitabu hiki, *Mwanasesere wa Mosi* kuwachochea watoto wa kiume kuamini kwamba katika kununuliwa 'magari' 'eropleni' na 'baiskeli' za kuchezea, wana uwezo mkubwa dhidi ya wenzao wa kike ambao vifaa vyao vya kuchezea ni wanasesere. Kadhalika, kuna uwezekano mkubwa wa watoto wa kike kubwia taswira dumifu ya uana kwamba ulezi ndilo jukumu lao kuu katika jamii. Kwa hivyo, taswira dumifu ya aina hii huchangia katika kukongomelea (fixate) mienendo ya watoto wa jinsia hizi pindi wanapokuwa watu wazima.

Katika hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi,* mama yake Mosi anakawia kimaksudi kumnunulia mwanasesere kwa sababu anataka amnunulie mwanasesere wa kipekee. Tunaelezwa kwenye hadithi:

> "Lakini Mama, kila siku unasema ningoje…"Mosi alilalamika kwa sauti ya kudeka. Alikuwa analengwalengwa na machozi. "Mwanasesere wa kipekee hapatikani kirahisi. Itabidi usubiri." "Mimi sikati wa kipekee Mama.Niletee tu kama wa Namsi au wa Kunda."Alisisitiza Mosi. Walipofika dukani, Mosi aliona mwanasesere mzuri akamwomba mama

amnunulie. Lakini Mama akasema, "Hakufai huyu Mosi. Huyu si wa aina yako." (Uk. 10&11).

Pindi mama yake anapomnunulia mwanasesere, Mosi anagundua upekee wa mwanasesere huyo kwamba anawafanana yeye na mama yake. Kufanana huku kunashadidia taswira dumifu ya uana ya ulezi katika jamii ambamo kazi hii imeibuka. Tofauti na Kunda na Namsi ambao wana wanasesere wasiowafanana, Kuna uwezekano mkubwa wa Mosi kuamini kwamba mwanasesere wake ni mtoto wa kweli kwa sababu ya kumfanana. Katika kumnunulia mwanasesere wa aina hiyo, mama yake Mosi anasisitiza umuhimu wa shughuli za ulezi kwa Mosi pindi atakapokuwa mtu mzima. Kwa hivyo anahakikisha kwamba binti yake ameibwia taswira hii ya uana.

### 3.3.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume

Takriban wahusika wote katika *Mwanasesere wa Mosi* ni wa kike isipokuwa baba yake Mosi. Wahusika wengine wa kiume hawatajwi kwenye matini, ingawa wanaonekana kwenye michoro. Kwa vile utafiti huu unajishughulisha na matini iliyoandikwa peke yake, hatuwatambui wahusika hao.

Kwa jumla, kuna wahusika saba wa kike katika hadithi hii. Hawa ni pamoja na Mosi (ambaye ni mhusika mkuu), Namsi na Kunda (Marafikize Mosi) Mama yake Mosi, Mama Mdogo Tina na Hawa ambaye ni mtoto yatima katika Makao ya watoto. Tulivyotaja hapo juu ni kwamba mhusika wa kiume wa pekee katika kazi hii ni baba yake Mosi. Hii ina maana kwamba mhusika wa kiume hajawakilishwa ipasavyo katika kazi hii.

### 3.4.0 *Mgomba Changaraweni*

### 3.4.1 Muhtasari wa *Mgomba Changaraweni*

*Mgomba Changaraweni* ni mojawapo ya kazi nyingi za kifasihi alizotunga Ken Walobora. Walibora anafahamika sana kama mtunzi wa riwaya na hadithi fupi ingawa pia ametoa mchango katika utanzu wa hadithi za watoto. Baadhi ya kazi zake ni pamoja na riwaya za *Siku Njema* (1996), *Kufa Kuzikana* (2003), *Ndoto ya Almasi* (2007). Vitabu vyake vya fasihi ya Kiswahili ya watoto ni pamoja na *Ndoto ya Amerika* (2001) *Mtu wa Mvua* (2004) *Chapuchapu* (2006) *na Mgomba Changaraweni* ambacho ni mojawapo ya kazi tunayoihakiki katika uctafiti huu.

*Mgomba Changaraweni* ni hadithi kuwahusu jagina mchunga mifugo anayeitwa Chongameno na msichana kwa jina Alice Kesho ambaye anampenda Chongameno. Chongameno kwa upande wake anakataa penzi la Alice. Hali hiyo inampelekea Alice kusababisha hasara na mateso makubwa kwa jamii yake kwa sababu Chongameno anakataa kumuoa. Moto aliouwasha ukateketeza msitu wa Suwerwa. Mwanzo, jamii yake inafikiria kwamba Chongameno ndiye mhalifu aliyetenda kosa hilo na kumtumbukiza gerezani. Mwishowe, inabainika kwamba kwa hakika Chongameno hana hatia kupitia kwenye ujumbe katika kijikaratasi alichoandika Alice kabla ya kujiua.

Hadithi hii ina sifa za vitabu vya fasihi ya watoto tulizotaja katika sura ya pili. Ina sura fupi, ni sahili na inasomeka kwa urahisi. Aidha ina michoro na imechapwa kwa maandishi makubwa na lugha sahili.

### 3.4.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Mgomba Changaraweni*

Taswira dumifu za uana katika *Mgomba Changaraweni* zinadhihirika hasa tunapoangazia hulka ya wahusika wakuu katika hadithi hii na majukumu yao ya kikazi. Chongameno ambaye ni mhusika mkuu na wa jinsia ya kiume amesawiriwa kama kijana mwenye nguvu aliyefanya kazi za ushokoa bila kuchoka. Picha ya Chongameno inayojitokeza katika hadithi hii inaendeleza taswira dumifu katika jamii kwamba mwanamume ni kiumbe mwenye nguvu na uwezo mkubwa wa kutenda mambo anapolinganishwa na mwanamke.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Alice Kesho kwa upande mwingine amesawiriwa kama kiumbe mrembo na safi anayependa kujirembesha kila wakati. Tunafahamishwa:

> Alisimama wima mbele ya kioo chake, kifua wazi alivyozaliwa. Aliyatazama kiooni madodo yake akayaona yameiva. Akacheka. 'Nani kama mimi?" akajisemea. Akajipaka mafuta mwilini. Ngozi yake ilikuwa laini. Hakuzoea kazi ya sulubu kama vijakazi wa pale nyumbani, waliojisaga kazini kama watumwa hasa. Haikuwa ajabu basi kuwa ngozi yake ilikuwa laini na nyororo. Alikuwa na umbo la wastani,si mwembamba sana si mnene sana,na ngozi yake ya maji ya kunde iliwapa vijana wavulana pumbao na tamanisho. (Uk. 19)

Vitabu vingi maarufu vya fasihi ya watoto (nchini Uingereza) huakisi taswira dumifu za uana kuhusu majukumu ya kazi kutegemea jinsia. Wahusika wa kike katika vitabu hivyo husawiriwa kuwa warembo (sweet) na wategemezi huku wahusika wavulana wakisawiriwa kuwa wenye nguvu na uwezo mkubwa wa kufanya mambo (Ernst, 1995; Jett-Simpson & Masland, 1993). Tunakubaliana na kauli ya wataalamu hawa ingawa wanazungumzia vitabu vilivyotungwa katika mazingira tofauti hasa kwa jinsi vinavyoingiliana na hulka za Chongameno na Alice Kesho katika *Mgomba Changaraweni.*

Hulka ya Alice Kesho kuwa mtegemezi wa Chongameno inajitokeza mwishoni mwa hadithi hasa anapoamua kujiua kwa sababu haoni maana ya maisha baada ya Chongameno kukataa ombi lake la kumtaka awe mpenzi wake. Hatua ya kujiua inazua maswali mengi kuliko majibu. Je, kulikuwa na haja ya Alice Kesho kujiua? Hatua hiyo inaonyesha kwa vyovyote udhaifu alio nao mwanamke kutoweza kuishi bila kumtegemea mwanamume?

Taswira dumifu nyingine ya uana inayobainika katika *Mgomba Changaraweni* ni kusawiriwa kwa Alice Kesho kama kiumbe laghai ambaye anaapa kutopumzika hadi anapohakikisha kwamba anamfunza adabu Chongameno kwa kukatalia mbali posa yake. Chongameno kwa upande wake amesawiriwa kama malaika ambaye hakasirishwi hata jamii inapomkosea kwa kumweka gerezani bila hatia. Kuhusu usawiri wa mwanamke kama kiumbe laghai tangu jadi, Momanyi (2001:24) anasema:

[...] Kwa upande mwingine, mwanamke amesawiriwa kama kiumbe laghai, mwovu, mzinifu na kigeugeu. Tunapochambua fasihi nyingi ulimwenguni, picha inayojitokeza zaidi [...] ni ile ya uovu wa mwanamke. Taswira hii pia ina chanzo chake katika mitazamo ya kidini, hususani ule uovu uliofanywa na Hawa kwa kumdanganya Adamu kula lile tunda lililokatazwa na Mungu [...] Taswira kama hizi ambazo aghalabu zinaumbwa na wasanii wa kiume hazitoki katika ombwe bali zina uhusiano wa moja kwa moja na historia na utamaduni wa jamii.[4]

(Msisitizo Wangu)

Ingawa mwandishi anatoka katika jamii ambapo kuna taswira dumifu kuwa wanaume ndio huwatongoza wanawake, anakiuka taswira hii dumifu ya uana na kutusawiria hali ambayo ni kinyume cha hayo. Alice ndiye anamtongoza Chongameno tena waziwazi. Itikadi ya taswira dumifu ya uana kwamba mwamamume ana mamlaka zaidi ya mwanamke inabainika katika barua ya Alice kwa Chongameno:

*Sahibu Chongameno,*

*Mbona unajirahisi hivyo? Unasema wewe maskini. Hilo mimi silikani. Lakini niambie: Ni mali gani iliyo na thamani bora zaidi ya adabu njema? Ni mali gani inayozidi utamu wa mapenzi bora? Umekataa katakata kunioa ati kwa sababu ya*

*ufukara wako. Lakini yakupasa ujue kuwa pendo la kweli halitegemei mali wala uluwa. Ninakuenzi kama mboni ya jicho langu. Nikikukosa sitakuwa na sababu ya kuishi. Una moyo safi na sera nzuri ya maisha. Dhumuni la barua hii ni kukuarifu kuwa nataka jibu lako mwisho uniambie kesho. Lau hunitaki kabisa kabisa na nia yako hutoghairi, nitatenda jambo nililolitaka na wengine wengi watadhurika.*

*Sahibu wako,*

*Alice Kesho* (Uk.13)

Katika barua hii, tunamwona Alice akimpigia magoti Chongameno kumwomba amwoe. Hii inatokana na taswira dumifu katika jamii kwamba wanaume wana mamlaka ya kuiongoza familia. Wahusika wengine katika hadithi hii wanaodhihirisha hali ya kuwa na mamlaka ni Mzee Masaba, ni mwajiri wa Chongameno ambaye pia ni tajiri sana. Nyadhifa za uhakimu na inspekta wa polisi pia zimeshikiliwa na wanaume. Ingawa hii ndiyo hali halisi nchini Kenya, kazi hii inaonyesha nafasi aliyo nayo mwanamume.

### 3.4.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume

Kazi hii haina usawa wa kiuana kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mhusika wa kiume amekwezwa hadhi katika nyanja hizi na mwenzake wa kike kudumazwa. Isitoshe wahusika wa kiume ni wengi kuliko wahusika wa kike.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumechunguza taswira dumifu za uana katika vitabu vilivyoandikwa na waandishi wa kiume (androtexts). Vitabu hivyo ni pamoja na: *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* (K.W. Wamitila, 2006), *Mwanasesere wa Mosi* (Demere Kitunga, 2002) na *Mgomba Changaraweni* (Ken Walibora, 2004) Kadhalika sura hii imeangaizia swala la uwakilishi wa wahusika wa jinsia ya kike na kiume katika vitabu hivyo.

Tathmini ya hadithi ya *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* imedokeza kwamba jamii inambagua mtoto wa jinsia ya kike kuhusu swala la urithi wa mali kutoka kwa baba yake – hasa urithi wa shamba. Kadhalika, imebainika kwamba, mhusika wa kike katika kazi hii, Koki amesawiriwa kuwa mtegemezi wa mhusika wa kiume kumuokoa, baba yake. Isitoshe wahusika wa kiume wamesawiriwa kuwa wenye nguvu na mamlaka zaidi kumshinda mhusika wa kiume. Kwa mfano, Ngoa na Gele wanatumia nguvu zao kumdhulumu dada yao na kumhini haki yake ya dawa ya majani ya mvinde. Hali hii ni mfano wa taswira dumifu iliyojikita katika jamii kwamba kwa sababu mwanamke ni kiumbe dhaifu asiyeweza kujitetea, watu wa jinsia ya kiume wanaitumia fursa hiyo kuwahini haki zao.

Imedhihirika pia kwamba majukumu waliyotengewa wahusika wa jinsia ya kike ni tofauti na yale ya jinsia ya kiume. Huku Koki akisawiriwa kama mlezi, myenyekevu na anayejali maslahi ya watu wengine, nduguze wa kiume wamesawiriwa kama watu wabinafsi. Aidha imebainika kwamba kuna idadi sawa ya wahusika wa kike na kiume katika hadithi hii

Hadithi ya *Mwanasesere wa Mosi* nayo imebainisha kwamba jamii hutoa mafunzo tofauti kwa watoto wa jinsia ya kike na kiume kwa minajili ya kuwaandaa kutekeleza majukumu yanayoenda sambamba na matarajio ya jamii hiyo pindi wanapokuwa watu wazima. Mosi kwa mfano anatarajiwa kuwa mlezi wa jamii kwa sababu jamii anamokulia inamtaka atangamane na majukumu hayo kwa kumkuza katika ulezi wa wanasesere. Kuhusu swala la uwakilishi wa wahusika wa jinsia tofauti, wahusika wa kike wameitawala hadithi hii.

Nayo tathmini ya hadithi ya *Mgomba Changaraweni* imeonyesha kwamba mtoto wa kike amesawiriwa kama kiumbe mlaghai ambaye amejifungata masombo kutopumzika hadi amwadhibu vikali mwenzake wa kiume kwa sababu ya ombi lake la penzi kukataliwa. Aidha, mhusika wa kike katika kazi hii, Alice Kesho anajiua hatimaye – ishara kwamba hawezi kuishi peke yake bila Chongameno. Hatua hii bila shaka ni kushadidia jinsi mwanamke alivyo mtegemezi wa mwanamume. Taswira ya mhusika wa kiume inayojitokeza katika hadithi hii ni kwamba ana mamlaka na uwezo dhidi ya mwenzake wa kike. Katika jamii halisi, si kweli kwamba wanawake wote ni walaghai. Aidha, hulka ya Chongameno kusawiriwa kama malaika asiyekuwa na dosari si picha halisi pia katika jamii zetu.

**Tanbihi**

1. Matiniume (androtexts) ni istilahi inayotumiwa kurejelea kinyume matininke (gynotexts). Kutokana na istilahi ya pili, tunapata istilahi 'gynocriticism' ambao ni uhakiki wa kazi zilizoandikwa na wanawake. Uhakiki huu ulianzishwa na Elaine Showalter mwishoni mwa miaka ya sabini na ulilenga kubaini kwamba waandishi wa kike wana mtindo wao wa kuandika unaotofautiana na mtindo wa waandishi wa kiume. Tatizo kuu la mtazamo huu ni kuwa ulitilia nguvu wazo la uegemezi wa kuumeni, kwamba sifa za ndani za kiuana ni za kiuasilia kutegemea jinsia.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

2. Mvinde (mara nyingine hutamkwa 'mvinje') ni mti mrefu wenye majani membamba sana yanayofanana na nyuzi na unaozaa matunda madogomadogo yenye vishimo vidogo.

3. Odhoji Benjamin (1997) ametoa maelezo ya kina kuhusu ruwaza zinazotutumika miongoni wa jamii ya Waluo katika kutofautisha majukumu ya watu wa jinsia tofauti, mahusiano ya kimamlaka na udhibiti wa raslimali miongoni mwa jamii ya Waluo.Taz. makala yake: 'Tradidional Bases of Sex Differentiation In Power Relations & Control of Resources: A study of Oral Folktales of Kanyango Clan of Masumbi, Among the Luo' In Wanjiku et al (ed) *Contesting Social Death: Essays on Gender & Culture*. Nairobi: KOLA. Pp. 39-59

4. Rej. Makala ya Clara Momanyi: 'Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Fasihi ya Kiswahili Baada ya 2000: Kuyimbisha Uhalisi' katika *Kiswahili 2000*. Dar Es Salaam: TUKI, p. 23– 33.

# SURA YA NNE

## TASWIRA DUMIFU ZA UANA KATIKA *NDOTO YA RIZIKI, SIKU YA WAJINGA* NA *ALITOROKA KWAO*

### 4.1 Utangulizi

Sura hii kama vile sura tatu, ni tahakiki ya fasihi ya Kiswahili ya watoto kubaini jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza katika kazi hizo. Tofauti ya sura hii na sura ya tatu ni kwamba, inashughulikia kazi zilizotungwa na waandishi wa kike, matininke[1] (gynotexts). Kazi hizo ni pamoja na: *Ndoto ya Riziki* (Razwana Kimutai, 2003) *Siku ya Wajinga* (Clara Momanyi, 2005) na *Alitoroka Kwao* (Angelina Mdari, 2001). Sababu ya kimsingi ya kuhakiki vitabu ambavyo vimeandikwa na waandishi wa kiume sambamba na tungo za waandishi wa kike ni kwamba, utafiti wenyewe unahusu maswala ya uana. Kwa hivyo, tunaamini kwamba kutathmini data kutoka kwa kazi za fasihi ya watoto za waandishi wa jinsia zote mbili kutatupatia matokeo yasiyokuwa na upendeleo wowote.

Hali kadhalika katika sura hii tunatathmini iwapo wahusika wa kike na kiume katika kazi hizi wamesawiriwa kwa misingi ya jinsia zao. Aidha katika sura hii kama tulivyofanya katika sura ya tatu, tunachunguza iwapo waandishi wa kazi hizi wanawakilisha kwa idadi sawa wahusika wa jinsia ya kike na kiume katika kazi hizi. Tathmini ya aina hii tulivyodokeza katika sura ya kwanza ni kwamba wasomaji hupendelea kujitambulisha na wahusika wa jinsia zao kwenye hadithi. Chambilecho Mem Fox (1993):

> Masuala ya jinsia katika fasihi yanaweza kuwa hatari kiasi kwamba yanaweza kuwadara wavulana na wasichana kubwia jinsi 'wanavyouona na kuufasiri ulimwengu' kwenye hadithi na hivyo basi kushadidia taswira dumifu za kiuana. Mshadidio huu unaweza kuwachochea watoto kutouliza maswali kuhusu mahusiano ya kiuana yaliyoko ya kijamii.[2]
>
> (Tafsiri Yangu)

### 4.2.0 *Ndoto ya Riziki*

### 4.2.1 Muhtasari wa *Ndoto ya Riziki*

*Ndoto ya Riziki* (2003) ni hadithi iliyotungwa na Razwana Kimutai. Huyu ni mwandishi chipukizi wa vitabu vya fani hii na hatufahamu kazi nyingine iliyowahi kutungwa na mwandishi huyu.

Hadithi hii ni kumbukumbu ya Bw Charo kuhusu ndoto ya bintiye, Riziki ya kuwa daktari. Bwana Charo anaikumbuka ndoto hii ambayo si ndoto tena miaka ishirini baadaye kwa sababu Riziki tayari ni daktari.

Katika udogo wake, Riziki anahuzunishwa na matatizo yanayoikumba familia yake. Mosi, mama yake, Bi Charo anaachishwa kazi yake ya uhazili katika hospitali moja mjini. Mapato ya Bw Charo kutokana na kazi yake ya useremala hayatoshi kukidhi mahitaji ya familia hii. Nduguye mdogo wa kiume, Tabu anaugua na kuteseka sana kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kugharamia matibabu yake. Hatimaye wanasaidiwa na jirani mwema, Bw Mateo ambaye anampeleka Tabu hospitalini kwa gari lake. Tukio hili

linamchochea Riziki kuamua kwamba, pindi akiwa mkubwa, atakuwa daktari. Uamuzi huo hata hivyo unatingwa na vikwazo vya hali ya ufukara ya familia yake. Hawezi kuhudhuria masomo shuleni kila siku na analazimika kuwa mlezi wa ndugu yake, Tabu kila mama yake anapokwenda kutafuta kazi. Siku moja, Riziki anapotumwa kwenda kuteka maji mferejini, anakutana na rafiki yake Hannah anayemkaribisha nyumbani kwao. Anapata fursa ya kumwelezea babake Hannah, Bw Mateo sababu zinazompelekea kutohudhuria masomo shuleni. Babake Hannah anamdokezea Riziki kwamba mama yake Hannah ambaye ni tabibu wa watoto anahitaji mhazili kumsaidia katika kliniki yake. Riziki anampasha habari mamake kuhusu kazi hiyo na habari zenyewe zinafungua njia ya ajira. Riziki anakwenda shuleni baadaye na juhudi zake masomoni zinamfanya afanikiwe kujiunga na shule ya upili na baadaye chuo kikuu ambapo anasomea utabibu na hatimaye kuwa daktari.

Kazi hii inaafiki sifa nyingi za vitabu vya fasihi ya watoto. Hadithi[3] ni sahili ila ploti[4] ni changamano kwa hadhira lengwa. Tunasema hivi kwa sababu ni vigumu kwa mtoto wa umri wa miaka kumi ( ambaye tunachukulia kwamba hadithi hii inalenga kwa sababu mhusika mkuu, Riziki ana umri huo) kutambua kwamba mwandishi anatumia kisengerenyuma) katika ploti ya hadithi hii.

### 4.2.2 Taswira Dumifu za Uana Katika *Ndoto ya Riziki*

Katika hadithi hii, mwandishi anadokeza wazi jinsi jamii pana kwa jumla inavyowachukulia watoto wa kike na kiume katika swala la elimu. Katika sura ya pili ambapo tumezungumzia kipengele cha uana na elimu, tumesema kwamba ingawa elimu ni muhimu, bado kuna ubaguzi mwingi wa vipengele kadha katika elimu ya nchini

Kenya. Tumesema kwamba hali hiyo imebainika katika viwango vya elimu kati ya watoto wa jinsia ya kike na jinsia ya kiume. Tumegusia pia kuwa katika uwanja wa taaluma wanawake wengi huwa katika taaluma zisizokuwa na ushindani mkubwa katika soko la ajira kama vile ualimu, uhazili n.k.

Aidha katika sura ya pili, tumesema kwamba, katika familia zisizokuwa na mapato ya kutosha, wazazi huamua kuwaelimisha watoto wavulana huku watoto wasichana wakibaki nyumbani na kufanya kazi za nyumbani. Kwa hivyo, elimu ya mtoto wa kike hutingwa na taswira dumifu baguzi ya utamaduni ya kumtaka abaki nyumbani kuwalea ndugu zao wachanga, kupika na kuteka maji miongoni mwa majukumu mengine. Taswira hii dumifu inajitokeza katika *Ndoto ya Riziki.* Mama yake Riziki anapokwenda mjini kutafuta kazi, anamkataza asiende shule kwa minajili ya kumlea Tabu, ndugu yake mdogo. Mwandishi anasema:

> "Riziki, leo usivae sare yako ya shule. Usiende shule kwa sababu naelekea mjini. Naenda kwenye mahojiano ya kazi. Itakubidi ubaki nyumbani umwangalie mdogo wako," Mama alimwagiza
> "mama, leo tena? Alinung'unika Riziki.Hii ilikuwa siku yake ya tatu juma hilo kuhudhuria shule.
> "Mama, unafahamu ninakosa siku nyingi kuenda shule? Kwa nini Baba hawezi kumtunza Tabu?" (Uk. 5)

Hali ni tofauti kwa mtoto wa kiume katika hadithi hii ambaye anahudhuria masomo kila siku bila kukosa hata siku moja. Haya yanadhihirika kupitia kwa wahusika wawili wa kiume, Bakunja na Mkesimume ambao walisomea shule moja na Riziki. Bakunja na Mkesimume wanamfanyia stihizai Riziki wanapomkuta akienda mferejini kuteka maji huku wao wakielekea shuleni, ingawa tunaambiwa kwamba Riziki alikuwa mwerevu masomoni kuwashinda. Hali hii inashadidia taswira dumifu katika jamii kwamba kumuelimisha mtoto wa kiume ni bora kuliko mtoto wa kike. Je hatima ya mtoto wa kike ni ipi katika hali kama hii?

Jibu la swali hili ni kwamba, mtoto wa kike ambaye amebaguliwa na taswira dumifu za uana kama Riziki anavyobaguliwa zinamfanya mtoto wa kike aamini kwamba ukombozi wake umo katika kupatiwa fursa sawa na ya mwenzake wa kiume kupata elimu na kufanya kazi katika taaluma inayoweza kumkimu na kumwepusha na ubaguzi wa jamii. Tunasoma kwenye hadithi:

> Alipokuwa njiani kuelekea mferejini kuteka maji, <u>Riziki aliwaza namna maisha yalivyo tofauti hasa kwa mtoto wa kike kama yeye.</u> Barabarani alikutana na watoto wanaoenda shuleni. Alijipa matumaini. Alifikiria...*Siku moja nitakapokuwa daktari mashuhuri, sitaenda tena kuteka maji! Nitakuwa na nyumba yangu kubwa yenye mifereji mingi ya kutosha.* "Mtazame kijakazi! Leo haendi shuleni," [...] aligutushwa kutoka njozi yake ya mchana na maneno haya ya Bakunja na Mkesimume.
>
> (Msisitizo Wangu)

Katika hadithi hii, taswira dumifu ya uana ambayo pia inajitokeza ni kwamba, jamii inaamini kwamba mtoto wa kike si sawa na mtoto wa kiume katika utendajikazi wa maswala fulani. Kwa sababu jamii inamwona mtoto msichana kama kiumbe dhaifu, ambaye hana budi kujitahidi maradufu kuithibitishia jamii kwamba ana uwezo wa kutenda yale ambayo mwenzake wa kiume anaweza kuyatenda. Katika *Ndoto ya Riziki*, watu wa jamii anamokulia Riziki wanatambua kwamba hata mtoto wa kike ana uwezo wa kutenda yale anayoweza kuyatenda mtoto wa kiume kutokana na jitihada zake. Tunaelezwa kwenye matini ya hadithi hii kwamba:

> Watu mtaani kwao watakwambia kuwa Riziki alipokuwa mdogo, aliweza kupanda mti mrefu pale mtaani. <u>Alifanya hivyo kuwathibitishia wavulana wa rika lake kwamba lile walilоweza kulifanya hata yeye msichana anaweza kulifanya</u>. Kwake yeye tofauti kati ya msichana ilikuwa inajulikana wazi. (Uk.1)
>
> (Msisitizo Wangu)

### 4.2.3 Majukumu ya Wahusika

Aidha, tofauti za majukumu katika jamii inayomkuza Riziki zinashadidia udhaifu anaochukuliwa kuwa nao mwanamke kutokana na majukumu ya kikazi anayotengewa kama inavyobainika katika kazi hii. Baba yake Riziki anafanya kazi ya useremala ambayo imenasibishwa na matumizi ya nguvu nyingi huku mama yake, Bi Charo akiwa mhazili. Kazi ya uhazili hunasibishwa sana na wanawake ambao hawajasoma. Kwa

hivyo, hatukosei kudai kwamba mwandishi anajaribu 'kufuta' taswira dumifu za uana katika jamii kuhusu taaluma na uwezo alio nao mtoto wa Kike kwa kumsawiri Riziki kama mhusika anayejitahidi kukwepa kazi za taaluma kama uhazili ambazo zina malipo duni na kusomea utabibu ambayo ni taaluma ya hadhi na yenye malipo mazuri. Licha ya juhudi na kujiamini kwa Riziki, jamii bado inaonekana kutilia shaka uwezo wake wa kuwa daktari: Tunaelezwa katika hadithi:

> Kuna jambo moja ambalo kila mtu mtaani kwao alikuwa analijua kumhusu Riziki. Riziki alikuwa na azma ya kuwa daktari. Waliijua nia yake kwa sababu Riziki alimwambia kila mtu aliyekubali kumpa masikio yake kumsikiliza. Watu wengi hasa marafiki zake shuleni walimcheka tu. Wengi waliyapuuza maneno yake kuwa ya mwotaji. Walimwona kama mtu anayeota vitu visivyowezekana kutokea. (Uk.2)

Udaktari ni taaluma inayohitaji mtu kusomea masomo ya sayansi hususan Kemia, Hisabati, Baolojia. Kuna taswira dumifu katika jamii hasa nchini Kenya kwamba ni wanafunzi wa kiume ndio wenye uwezo wa kumudu masomo haya, tofauti na wenzao wa kike. Wakishadidia kauli hii, Okere na Keraro (2002: 140) wanakubali kwamba taswira dumifu za uana zilizojikita katika tamaduni za baadhi ya jamii nchini Kenya huathiri ujifunzaji wa masomo ya sayansi hasa wakati wa utotoni.

Shaka ya jamii kuhusu uwezo alio nao Riziki wa kusomea taaluma ya udaktari huenda inatokana na imani kwamba, yeye ni mtoto wa kike ambaye hawezi kumudu masomo yanayochangia katika kumwezesha mtu kuwa daktari na pili, kwamba taaluma hii ni ya wanaume. Hata hivyo, mwandishi wa kazi hii amechukua hatua ya kimakusudi 'kufuta' taswira hii dumifu ya uana kwa sababu Riziki na Bi Mateo ni madaktari. Hii inaonyesha kwamba taswira hiyo dumifu ya uana haina mashiko ila tu ni kikwazo cha bure kwa mtoto wa kike.

### 4.2.4 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume

Katika hadithi ya *Ndoto ya Riziki*, mwandishi amemtumia mhusika mkuu wa kike kimaksudi kuonyesha uwezo mkuu anaoweza kuwa nao mtoto wa jinsia hiyo iwapo anajiamini na kufanya bidii. Kwa jumla, mwandishi ametumia idadi sawa ya wahusika wa kike na kiume katika kazi hii. Wahusika wa kike ni pamoja na Riziki ambaye ni mhusika mkuu, Mama yake, Bi Charo, Juna ambaye ni rafiki ya Riziki katika chuo kikuu na Bi Mateo ambaye ni daktari. Wahusika wa kiume ni pamoja na Bw Charo ambaye ni baba yake Riziki, Bw Mateo ambaye baba ya Hannah na Tabu, ndugu mdogo wa Riziki na Bakunja na Mkesimume wanaosoma shule moja na Riziki.

## 4.3.0 *Siku ya Wajinga*

### 4.3.1 Muhtasari wa *Siku ya Wajinga*

*Siku ya Wajinga* ni mojawapo ya kazi za kisanaa za Clara Momanyi. Momanyi ni mtunzi wa hadithi fupi na riwaya za vijana. Baadhi ya tungo zake ni *Ngome ya Nafsi* (hadithi

fupi katika mkusanyo wa *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, 2004) na *Tumaini* (2006) ambayo ni riwaya ya vijana.

Jagina katika kazi hii ni Zito ambaye ni mwanafunzi katika shule ya Msingi ya Kambini. Zito ni mtundu na mwenye mizaha mingi darasani. Tofauti na rafikize, Sadiki na dada yake Zena ambao ni wenye bidii za mchwa masomoni, Zito ni mvivu. Mienendo hii yake inamtia matatani kila mara na kusababisha aadhibiwe na wazazi wake na walimu mara kwa mara.

Zito ana falsafa kwamba 'werevu ukikushinda jaribu ujinga'. Katika kuitetea falsafa yake hii, Zito anafanya juhudi kuwashawishi wanafunzi wenzake kuamini kwamba mtu mwerevu daima humtumikia mtu mjinga. Zito ameukumbatia ujinga kwelikweli.

Kwa sababu ya uzembe wake, Zito hang'amui somo la Hisabati wala hataki kuonyeshwa na wanafunzi wenzake wanaojitolea kumwonyesha somo hilo hasa wasichana. Licha ya kutopenda somo hilo, Zito pia hampendi mwalimu Petro ambaye analifunza somo lenyewe. Mwalimu Petro anamwadhibu Zito mara kwa mara kwa sababu ya kufeli somo hilo.

Adhabu zinapochacha, Zito anaamua kutafuta njia ya mkato kujiokoa kutokana na adhabu ngumu ya kung'oa visiki. Jioni walimu na wanafunzi wote wanapokuwa uwanjani kuona mazoezi ya mchezo wa kandanda, ananyapianyapia hadi afisini kwa mwalimu Petro na kuiba majibu ya zoezi la Hisabati walilopewa darasani. Siku

inayofuatia, Zito ndiye wa kwanza kumkabidhi mwalimu kitabu asahihishe. Kwa ujinga wake, hajui kwamba njia ya mwongo ni fupi. Majibu ya zoezi hilo ni sahihi ila hakuonyesha alivyoyapata. Haepuki adhabu ya kufyeka nyasi zote kwenye uwanja wa mpira.

Zito ni mhusika anayependa vituko na mwenye kuthubutu (adventurous). Anapoadhibiwa na Mwalimu Rukia kwa kuimba kwa sauti kama ya chura darasani wakati wa somo la Mziki, anaamua kujilipizia kisasi kwa kumshtua mwalimu huyo wanapokuwa wanatoka shule ya Mkomani kuhudhuria mchezo wa kandanda. Anarusha bungo majini kutoka kwenye mti alioukwea na kucheka kicheko kama sokwe ambacho kinamshtua mwalimu Rukia aliyekuwa anapitia sehemu ya makaburini alipokuwa akitoka shule ya Mkomani kuhudhuria mchezo wa mpira.

Vituko vya Zito vinafikia kileleni anapoambiwa amkamate jogoo na mama yake. Anamfukuza jimbi huyo hadi kwa Mzee Lombo ambapo jimbi anaruka juu na kuingiza miguu yake kwenye kitoweo cha mzee huyo aliyekuwa akila. Mambo yanachukua mkondo tofauti jioni moja Zito anapojaribu kuwaingiza zizini mifugo wa wazazi wao. Fahali wao mmoja, Mapaku anadinda kuingia zizini na kumlazimu Zito kumkuna shingo na mgongoni. Mapaku anaudhika na kuanza kutimua mbio. Kwa ujinga wake, Zito anaukwamilia mkia wa fahali huyo na hatimaye kuanguka na kuumia vibaya sana na kulazwa hospitalini.

Walimu na wanafunzi wanaokuja kumfariji hospitalini wanamcheka kwa sababu ya ujinga wake uliosababisha ajali hiyo. Zito anaamua kujilipizia kisasi kwa kusubiri Aprili Mosi (Siku ya Wajinga) ifike. Siku hiyo inapofika, anawadanganya wanafunzi wote shuleni na kuhatarisha maisha yao. Anatimuliwa kutoka shuleni na hatimaye kujipata katika shule maalum ya kurekebisha tabia za watoto watundu ambapo anajaribu kutoroka lakini mlinzi anamwona.

Miaka miwili baadaye, Zito anagundua kwamba falsafa yake ya kuukumbatia ujinga haiwezi kumsaidia chochote. Baada ya tabia yake kurekebishwa, anarudi katika shule yake ya zamani ya Kambini ambapo anaiaga falsafa yake na kuibuka na nyingine kwamba 'Ukitaka cha Mvunguni, Sharti uiname'. Lakini wenzake tayari wamekwisha kupiga hatua masomoni na kujiunga na shule za upili.

*Siku ya Wajinga* ni hadithi ya kuvutia ambayo pia inaafiki sifa za vitabu vya fasihi ya watoto. Hadihti na ploti ni sahili, lugha ni nyepesi na ina mvuto wa aina yake.

### 4.3.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Siku ya Wajinga*

Taswira nyingi dumifu za uana katika kazi hii zinadhihirika kupitia kwa mhusika mkuu, Zito. Kama ambavyo tumetaja kwenye muhtasari wa hadithi ya *Siku ya Wajinga*, mwandishi amemsawiri mtoto wa kiume kuwa mpenda vituko na mwenye kuthubutu kufanya mambo. Fauka ya hayo, Zito ni mwasi anapolinganishwa na mhusika wa kike katika kazi hii, Zena ambaye ni mtiifu kwa wazazi wake.

Kupitia kwa Zito, tunabaini taswira nyingine dumifu ya uana iliyosakini katika jamii inayomkweza hadhi mtoto wa kiume na kumweka pembezoni mtoto wa kike. Katika *Siku ya Wajinga*, Zito ambaye ni mvulana amekuzwa na jamii inayoamini kwamba ni udhaifu mwanamume kuonyeshwa jambo na mwanamke. Pamoja na hayo, ina maana kwamba, jamii ambamo kazi hii imeibuka imemlea mtoto wa kiume kwenye utamaduni unaoshadidia kwamba mwanamume anapaswa kuwa mjuzi wa kila jambo na kwamba inapotokea kwamba hajui, basi ni udhaifu kukubali uonyeshwe jambo hilo na mwanamke. Tunasoma kwenye hadithi:

> Zena alijitolea kumsaidia (*Zito*) kulielewa somo hili (*hisabati*), lakini Zito hakupenda kuonyeshwa hesabu na wasichana. Aliona haya sana kila aliporekebishwa na Zena au msichana mwingine mle darasani.(Uk.13)
>
> (Maneno ya mlazo na msisitizo ni wangu)

Taswira hii dumifu ya uana ina madhara yake kwa mtoto wa kiume kwa sababu hatimaye inamdhuru Zito. Ni kweli kwamba Zito anatambua wazi kuwa ana udhaifu katika somo la Hisabati. Hana moyo wala azma ya kutaka Zena (msichana) amwonyeshe jinsi ya kufanya hesabu, kwa sababu ya jamii anamokulia inachochea taswira dumifu ya uana kwamba mwanamume hapaswi kuonyeshwa jambo na mwanamke inamharibia maisha Zito. Isitoshe, somo la Hisabati linachukuliwa kuwa la wavulana peke yao kama tulivyoona katika *Ndoto ya Riziki*. Tunaambiwa kwenye hadithi:

> (*Zito*) Aliona haya sana kila aliporekebishwa na Zena au msichana mle darasani. Hata hivyo, Sadiki alimweleza kuwa somo la hesabu sio la wavulana pekee, kwa hivyo asione haya ya kuelekezwa na wasichana. Haya hayakumpendeza Zito. Kwake kuelekezwa na wasichana kulikuwa dharau kubwa. [...] (*Zito anapokubali kuonyeshwa hesabu na Zena, anatoa masharti kwamba msaada huo utolewe faraghani*) zito alitazama huku na huko, kisha akamwambia kwa sauti ya chini, "Hapana sio sasa. Nionyeshe wakati wa breki." (Uk.13)
>
> (Maneno ya mlazo na Msisitizo ni Vyangu)

Mwandishi wa *Siku ya Wajinga* pia ameangazia swala la taswira dumifu za uana zinazodhihirika kupitia kwa ugavi wa majukumu ya kikazi kati ya wanawake na wanaume na watoto wasichana na wavulana. Katika kipengele hiki, Momanyi anajaribu kimaksudi kufuta mpaka huu hasa kupitia kwa wahusika wawili mapacha, Sadiki na Zena. Mwandishi anaonekana kupinga taswira dumifu katika jamii ambapo mtoto wa kike ananasibishwa na kazi za nyumbani kama vile kusafisha vyombo, kufagia nyumba, kupika miongoni mwa majukumu mengine. Katika kuwachora wahusika hawa kuwa mapacha, Momanyi anaashiria kwamba mtoto wa kike na kiume ni sawa na hivyo basi jamii haipaswi kumkweza hadhi mmoja na kumwacha mwengine. Tunasoma kwenye hadithi:

> Sadiki na Zena walikuwa pacha.[...] Pacha hawa walishirikiana katika mambo mengi.[...] Walisaidiana pia katika kufanya kazi za nyumbani bila kujali maumbile yao. Sadiki alipokuwa akimsaidia mama yao kusafisha vyombo, Zena angekimbilia ufagio akafagia nyumba yao yenye vyumba vine. Wazazi wao daima waliwafundisha kushirikiana na kutochagua kazi. [...]Mama yao aliwafunza mapishi mbalimbali, usafi wa nyumba na ufuaji nguo pia.[...]Walifunzwa kupalilia mimea mbalimbali na kuvuna. Walifunzwa kuwakama ng'ombe na kuwachunga wakiwa malishoni. (Uk 7-8)
>
> (Msisitizo Wangu)

Kutokana na dondoo hili kuna majukumu yanayofaa kutekelezwa na wanaume au wavulana na yale ambayo jamii iliyowatengea wanawake au wasichana. Majukumu ambayo jamii imewatengea wavulana au wanaume katika dondoo hili ni pamoja na kuchunga mifugo malishoni. Majukumu ya kikazi yaliyotengewa mtoto wa kike au mwanamke ni pamoja na kusafisha vyombo, kufagia nyumba, kuwakama ng'ombe, kupika na usafi wa nyumba kwa jumla. Kwa hivyo, hatukosei kusema kwamba mtoto wa kike hukabiliwa na kazi nyingi kushinda mwenzake wa kiume na huu ni ubaguzi.

Wazazi wa Sadiki na Zena wanapohakikisha kwamba wana wao wanafanya kazi sawa bin sawa, wanajaribu kufuta taswira dumifu ya uana na kuleta usawa katika jamii. Kadhalika, mwandishi anaonyesha kwamba haidhuru kwa vyovyote vile mtoto wa kiume kutekeleza majukumu yaliyotengewa mtoto wa kike kama vile kumsaidia mama kusafisha vyombo na mtoto wa kike kuwachunga mifugo.

Licha ya kupigania usawa huo kwa upande wa majukumu, mwandishi wa kazi hii amemsawiri mtoto wa kiume kuwa na nguvu nyingi na hivyo basi kuweza kufanya kazi ngumu kama vile kung'oa visiki vya miti, kufyeka nyasi. Kila Zito anapoanguka hesabu, anaadhibiwa kwa kupewa kazi hizo.

Kadhalika, katika kumsawiri mtoto wa kike kuwa mweledi katika masomo na hasa somo la Hisabati na mwenzake wa kiume kuwa zuzu katika somo hilo, mwandishi anajaribu kufuta taswira dumifu iliyosakini katika jamii kwamba mtoto wa kiume anamudu masomo ya sayansi zaidi kuliko mwenzake wa kike (Okere na Keraro: ibid)

Aidha, taswira dumifu ya uana kuhusu ukuruba anaokuwa nao mtu na mama yake ambaye anamlea inajitokeza katika kazi hii. Zito anapokuwa akijaribu kutoroka kutoka shule maalum alikopelekwa kurekebishwa tabia, anakamatwa na mlinzi. Katika mkimkiki huo, Zito anaangua kilio huku akisema.

> Niache niende...niache. Mamangueee!" Zito alianza kulia na kutupatupa miguu na mikono hewani. (Uk.59)
>
> (Msisitizo Wangu)

Ingawa Zito ni mvulana ambaye anatarajiwa na jamii kuhimili machungu bila kulia, tunamwona akiangua kilio anapojipata mashakani na isitoshe, kumlilia mama yake. Hii inaonyesha kwamba, athari ya ulezi na ukuruba anaokuwa nayo mtu na mama yake hujitokeza bayana kwa wanaume licha ya kuwepo taswira dumifu za uana katika jamii

halisi kumtaka mvulana au mwanamume kuvumilia mateso kiume bila malalamiko yoyote.

### 4.3.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume

Mwandishi wa *Siku ya Wajinga* ametumia idadi kubwa ya wahuska wa kiume kuliko wahusika wa kike. Mhusika mkuu, Zito ni wa kiume. Wahusika wengine wa jinsia hii ni pamoja na babake Zito, Sadiki, rafiki yake zito, Mzee Lombo, Mwalimu Petro, Mwalimu Timami na mlinzi katika shule maalum ya kurekebisha tabia. Wahusika wa kike ni pamoja na Zena ambaye ni pacha mwenza wa Sadiki, Mwalimu Rukia na mamake Zito.

## 4.4.0 *Alitoroka Kwao*

### 4.4.1 Muhtasari wa *Alitoroka Kwao*

Angelina Mdari ni mmojawapo wa watunzi maarufu wa hadithi za watoto nchini Kenya. Mbali na *Alitoroka Kwao*, mwandishi huyu ametunga vitabu vingine vingi. Baadhi ya kazi zake ni pamoja na *Visa vya Jumbe A*, *Visa vya Jumbe B*, *Yalianza Kimchezomchezo* na *Waliponea Chupuchupu.*

Katika hadithi ya *Alitoroka Kwao*, mhusika mkuu, Eva ambaye ni msichana mwenye umri wa miaka kumi na mitatu anashindwa kustahimili malezi mabaya ya Richard, baba yake wa kambo, ambaye anamfumania akikiri kwa mama yake, Roda kwamba hampendi. Isitoshe baba huyu wa kambo hathamini elimu ya mtoto huyu wa kike kwa sababu anakataa kulipia karo. Tunaelezwa kwamba Eva hamjui babake halisi na amekuwa akilelewa na nyanya yake na jamaa zake wengine ambao wanamwona kama mzigo. Hali hii inamfanya akue kwa mateso na kumfanya amchukie mama yake, jamaa zake na ukoo

mzima kwa jumla. Eva anafunganya virago na kutoroka nyumbani kwenda jijini Nairobi kwa kutumia nauli ya pesa alizoiba huku akiapa kutorudi mahala hapo tena.

Asichojua Eva ni kwamba jiji lina hatari nyingi kwa sababu hamjui jamaa yeyote katika jiji hilo. Kwa bahati nzuri, anakutana na Sista Agatha, mtawa ambaye alikuwa amekwenda kijijini kuwasalimia wazazi wake. Sista Agatha ambaye pia anaishi Nairobi anaamua kumsaidia Eva pindi wanapofika Nairobi. Anampeleka hadi kwa dada yake, Bi Mdamu ambapo Eva anaajiriwa kazi ya uyaya.

Eva anatangamana na marafiki wengine wasichana mtaani ambao pia ni watumishi na wasaidizi wa nyumbani. Hatimaye wanampotosha licha kwamba Bi Mdamu amemwonya kujiepusha na marafiki hao waovu. Anadanganywa na marafiki hao kwamba wana uwezo wa kumtafutia kazi nzuri kwingine na Eva anashawishika na kuondoka kwa mwajiri wake, Bi Mdamu bila kuaga, na kwenda kwingine ambapo pia anaajiriwa kazi ya uyaya.

Maisha ya jiji yanapozidi kuwa magumu, Eva anafanya kazi ya uyaya kwa miezi sita na kuamua kutafuta kazi kwenye baa na vilabu vya kuuzia pombe. Ni katika mahala hapa ambapo anakutana na Joni, mwanamume anayeahidi kumwoa. 'Ndoa' kati ya Joni na Eva ni ya masafa mafupi kwani baada ya mwaka mmoja wanafarakana. Akiwa katika njia panda baada ya mafarakano hayo, Eva anapashwa habari na mwanamke mmoja kwamba Joni ni mtu hatari ambaye ana virusi vya ukimwi; na kwamba kafiwa na wake zake watatu kwa sababu ya maradhi hayo.

Eva anatoroka kutoka kwa Joni na kwenda kwa Sista Agatha na baadaye kwenda kwa mwajiri wake wa kwanza, Bi Mdamu. Hatimaye anamalizia kufanya kazi katika makao ya watoto mayatima baada ya kubainika kwamba hata yeye kaambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

### 4.4.2 Taswira Dumifu za Uana katika *Alitoroka Kwao*

Katika kazi hii, taswira dumifu ya uana inayotawala ni jukumu la ulezi analotwikwa mtoto wa kike na jamii. Tulivyotaja katika sura ya pili ya utafiti huu ni kwamba tamaduni za Kiafrika humchukulia mtoto wa kiume kuwa wa hadhi ya juu anapolinganishwa na mwenzake wa kiume. Katika uhakiki wetu wa *Ndoto ya Riziki*, imebainika kwamba inapotokea kuwa familia haina mapato ya kutosha kuwaelimisha watoto wake wa kike na kiume, mtoto wa kiume aghalabu hupewa kipaumbele na mwenzake wa kike kulazimika kubaki nyumbani kutekeleza majukumu ya nyumbani kama vile malezi ya ndugu zao wadogo. Eva anajipata katika hali hii wazazi wake wanapokataa kumlipia karo kumwezesha kuendelea na masomo. Eva anamweleza Sista Agatha:

> "Nimetoroka nyumbani kwa sababu baba yangu wa kambo hanipendi, mama yangu mzazi hanipendi na nyanya pia hanipendi [….] Siendi shule mpaka muhula ukaisha. Kila mara hurudishwa nyumbani kwa ajili ya karo.'' (Uk.8&9)

Akiangazia swala hili, Momanyi (2003:8) anasema kuwa, jamii haina budi kutupilia mbali desturi na mila zinazomnyima mtoto wa kike nafasi ya

kujiendeleza maishani. Tamaduni zinazombagua na kumnyima elimu, au zile zinazomlazimisha kuolewa mapema, kumzuia kuvitumia vipawa vyake kama binadamu lazima zipigwe vita kwa manufaa ya jamii. Maoni ya Momanyi yanaafiki hali anayojipata Eva ya kutopewa haki yake ya elimu na hatimaye kulazimika kuolewa mapema na Joni.

Kutokana na kutothaminiwa na jamii, na kuonekana kama mzigo, Eva ni kielelezo cha wasichana wengi ambao hulazimika kutorokea mijini kutafuta ajira ambapo wanaajiriwa kazi duni ya uyaya: Tunaambiwa:

> Eva alipata kuajiriwa na familia moja iliyoishi mbali kidogo na kwa Bi Mdamu. Familia hiyo ilihitaji sana mtumishi wa kuwasaidia pale nyumbani. Kulikuwa na mtoto mchanga. Alihitaji kuangaliwa wakati mama na baba yake walipokwenda kazini.[...]Walimwajiri na kumpa ahadi ya mshahara mnono. (Uk. 30)

Kwa sababu ya malipo duni, Eva hana budi kutafuta njia nyingine za kujikimu kimaisha. Hali hii inamlazimisha kwenda kutafuta kazi kwenye baa na vilabu vya kuuzia pombe ambapo alianzisha urafiki na mwanamume mmoja, Joni.

Taswira dumifu ya uana inayobainika kupitia kwa mahusiano ya Joni na Eva ni kwamba mtoto wa kike ni chombo cha kukidhi uchu wa mwanamume. Joni ni kielelezo cha

wanaume katika jamii pana wanaowahadaa wasichana wadogo na kuwadhulumu na kuwaharibia maisha yao. Tunasoma kwenye hadithi:

> Mtu huyo alikuwa na umri wa miaka thelathini.[...]Eva mimi ninakupenda zaidi ya kitu chochote ulimwenguni! Ninataka nikuoe uwe wangu milele!' Mwanamume akasema. [...] Msichana wetu hakuwa ameambiwa na mtu yeyote ati 'anampenda' tangu kuzaliwa kwake. Msichana akaamini. (Uk.31-32)

Kutokana na dondoo hili tunabaini hatari zinazomkabili mtoto a kike ambaye hapati malezi mema. Kutokana na misukosuko ya familia ya Eva ambaye hata hamjui baba yake halisi, msichana huyu hapati malezi thabiti ya kumsaidia kubaini watu waongo na wanaosema ukweli, mabaya na mazuri. Joni, ni kiwakilishi cha wanaume malofa ambao hatimaye wanamharibia maisha msichana huyu mdogo na mbichi.

### 4.4.3 Uwakilishi wa Wahusika wa Kike na Kiume

Mwandishi wa kazi hii ametumia idadi kubwa ya wahusika wa kike kuliko wahusika wa kiume. Wahusika wa kike ni pamoja na Eva ambaye ni mhusika mkuu, mama yake Eva, Roda, Sista Agatha na dada yake Bi Mdamu, nyanya yake Eva. Wahusika wa kiume ni baba wa kambo wa Eva na Joni.

## 4.0 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili na kutoa mifano kutoka kwenye matini za fasihi ya watoto iliyotungwa na waandishi wa kike ili kubainisha jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza katika kazi hizo. Aidha, sura hii imeangazia pia swala la uwakilishi wa wahusika wa jinsia zota katika kazi hizo.

Katika hadithi ya *Ndoto ya Riziki*, taswira dumifu ya uana inayojitokeza wazi ni jinsi mtoto wa kike anavyonyimwa haki ya kusoma kwa sababu ya kufanywa mlezi na mfanyakazi wa nyumbani karo ya kumpeleka shuleni inapokosekana. Mtoto wa kike anayejipata katika hali hii anaamini kwamba elimu ndiyo nyenzo ya kumkomboa kutokana na hali hiyo.

Aidha, taswira hii dumifu pia imejitokeza katika *Alitoroka Kwao* ambapo mtoto wa kike anaajiriwa kazi ya uyaya yenye mshahara duni. Hali hiyo inasababisha awe chambo cha wanaume wenye pesa ambao wanamharibia maisha yake.

Katika kazi hizi mbili, wahusika wa kike ndio wahusika wakuu. Idadi ya wahusika wa kike na wa kiume inalingana katika *Ndoto ya Riziki*. Katika *Siku ya Wajinga* wahusika wa kiume ni wengi kuliko wahusika wa kike ilihali wahusika wa kike ni wengi katika *Alitoroka Kwao.*

## Tanbihi

1. Matininke (gynotexts) ni istilahi inayotumiwa kurejelea kinyume cha matiniume (androtexts). Kutokana na kwanza, tunapata istilahi 'gynocriticism' ambao ni uhakiki wa kazi zilizoandikwa na wanawake. Uhakiki wa aina hii ulianzishwa na Elaine Showalter mwishoni mwa miaka ya sabini na ulilenga kubaini kwamba waandishi wa kike wana mtindo wao wa kuandika unaotofautiana na mtindo wa waandishi wa kiume. Tatizo kuu la mtazamo huu ni kuwa ulitilia nguvu wazo la uegemezi wa kuumeni, kwamba sifa za ndani za kiuana ni za kiuasilia kutegemea jinsia.

2. Pindi tu mtoto anapozaliwa huainishwa kuwa ama ni 'mvulana' au 'msichana' na uainisho huu unaathiri majukumu ambayo mtoto anatarajiwa kuteiekeza. Kwa hivyo, jinsi anavyokua, mtoto hukumbana na dira kadha za kumuongoza katika kutimiza majukumu mbalimbali kulingana na jinsia yake. Dira hizi ni pamoja na wazazi, ndugu zake, shule, runinga, vitabu n.k. Hata hivyo, mienendo kadha inayochukuliwa kuwa inafaa mtoto wa jinsia fulani inasheheni taswira dumifu ambazo haziakisi uhalisia wa maisha. Taz. Mem Fox 'Men Who Weep, Boys Who Dance: The Gender Agenda Between the Lines in Children's Literature' In *Language Arts* pp. 84-88.

3. Hadithi ni dhana inayotumiwa kuelezea mfululizo wa matukio kwa kuzingatia au kutilia maanani mfuatano au mpangilio wake kiwakati. E.M Forster ametoa mfano kuwa: chajio huja baada ya chamshakinywa, Jumanne huja baada ya Jumatatu na kadhalika. Taz. *Aspects of The Novel*. Penguin Books, 1927. Uk.29

4. Ploti ni mtiririko (mfuatano, mfululizo) wa matukio yanayoijenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana. Katika hadithi ya *Ndoto ya Riziki* ni vigumu msomaji chipukizi kufuatilia matukio kiusababishi kwa sababu mwandishi ametumia mbinu rejeshi ambapo Bw Charo anakumbuka ndoto ya bintiye Riziki miaka 20 baadaye. Hadithi za watoto huhitaji ploti sahili.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunawasilisha hitimisho la utafiti wetu. Sura hii ina sehemu zinazoshughulikia matokeo ya utafiti, nadharia tete, matatizo tuliyokumbana nayo wakati wa utafiti huu na mapendekezo ya utafiti zaidi katika swala la taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto.

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Kwenye tasnifu hii tuliazimia kuchunguza jinsi taswira dumifu za uana zinavyojitokeza katika baadhi ya vitabu vya fasihi ya Kiswahili ya watoto. Lengo letu kuu lilikuwa ni kuchunguza ni kwa kiwango na kwa namna gani waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wanaendeleza taswira dumifu za uana zinazoendeleza ubaguzi wa kijinsia. Je, uendelezaji huu ni jambo linalofanywa kimaksudi au ni sadfa? Kadhalika tulikuwa na nia ya kutathmini iwapo wahusika wa kike na wa kiume katika fasihi hiyo wamesawiriwa kwa usawa au iwapo wamebaguliwa kwa misingi ya jinsia zao. Lengo kuu la madhumuni haya lilikuwa ni kuonyesha kwamba kutosawiriwa kwa wahusika kwa njia ya usawa katika fasihi ya watoto kunaweza kuchangia katika kuendeleza taswira dumifu za uana katika jamii husika.

Tumegundua kwamba waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wanaendeleza taswira dumifu za uana. Kutokana na matini za kazi za fasihi ambazo tumezihakiki, mhusika wa kike amesawiriwa kuwa dhaifu, mtulivu, mlezi, mtegemezi wa mwenzake wa kiume

huku mhusika wa kiume akisawiriwa kama mwenye nguvu, mwenye kuthubutu (adventurous) na uwezo mkubwa wa kufanya mambo.

Uchunguzi huu pia umegundua kwamba mhusika wa jinsia ya kike amebaguliwa katika maswala ya urithi wa mali hasa ardhi pamoja na kunyimwa haki ya kwenda shuleni. Inapotokea kwamba familia yake haina mapato ya kutosha kama tulivyoona katika *Ndoto ya Riziki*, mtoto wa kike analazimika kubaki nyumbani kuwa mlezi na mfanyakazi za nyumbani ilhali mwenzake wa kiume anakwenda shuleni. Hali hii inatokana na taswira dumifu za uana zilizokita mizizi katika jamii ambamo kazi hizi zimeibuka. Taswira hizo za uana zinamkweza hadhi mtoto wa kiume na kumdumaza wa kike.

Kuhusiana na swala la taswira dumifu baguzi za uana, uchunguzi wetu umedokeza kwamba baadhi ya taswira dumifu za uana ni kikwazo kikubwa kwa mtoto wa kike katika hatua yake ya kujiendeleza kitaaluma. Jamii ambamo waandishi wa kazi ambazo tumezihakiki wanatoka zinaamini kwamba mtoto wa kike hana uwezo wa kumudu masomo kama hisabati na mengine katika taaluma ya sayansi. Taswira hii dumifu ya uana si kweli kwa sababu mhusika Zito katika *Siku ya Wajinga* hang'amui hisabati, na hataki kuonyeshwa na msichana kwa sababu ya taswira dumifu kwamba msichana akikuonyesha hisabati, huo ni udhaifu. Mhusika Riziki katika *Ndoto ya Riziki* ni msichana ambaye hana budi kupambana na taswira dumifu ya aina hiyo ili kuwa tabibu. Mhusika Eva katika *Alitoroka Kwao* anajipata kanaswa na taswira dumifu ya uana ya kutolipiwa karo ya shule kwa sababu yeye ni msichana na wazazi wake ni maskini. Anatorokea mjini ambapo anaajiriwa kazi ya uyaya ambayo ni duni.

Uchunguzi huu pia umegundua kwamba baadhi ya watunzi wa kazi za fasihi ya watoto ambazo tumezihakiki wanafanya juhudi za kimaksudi 'kufuta' taswira dumifu za uana katika kazi zao hasa kwa kumkweza hadhi kimaksudi mhusika wa kike ili awe sawa na mhusika wa kiume. Katika *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake*, mwandishi K.W. Wamitila ametamatisha hadithi hiyo kwa kukiuka taswira dumifu ya uana katika jamii ambamo kazi hiyo imeibuka kwamba, mtoto wa kike hawezi kurithi shamba. Koki mwishowe anarithi shamba la baba yake sawa na nduguze wawili wa kiume, Gele na Ngoa. Vilevile, katika *Siku ya Wajinga*, mwandishi Clara Momanyi amempa Zena (mhusika wa kike) uwezo wa kumudu somo la hisabati kumshinda Zito (mhusika wa kiume). Hatua ya kuwasawiri Sadiki na Zena kuwa mapacha na kutekeleza majukumu sawa ya nyumbani bila kujali maumbile yao ni hatua ya kimaksudi kuonyesha kwamba jamii zetu hazipaswi kuwalea watoto kwa kuegemea misingi ya taswira dumifu za uana.

Uchunguzi huu pia umegundua kwamba waandishi wa kazi tulizozihakiki hawawakilishi kwa idadi sawa wahusika wa kike na kiume. Kati ya kazi sita tulizozichunguza katika utafiti huu, ni mbili tu zilizokuwa na idadi sawa ya wahusika wa kike na wa kiume. Hizi ni pamoja na *Msichana Mlemavu na Ndugu Zake* (K.W. Wamitila) na *Ndoto ya Riziki* (Razwana Kimutai). Katika *Siku ya Wajinga* (Clara Momanyi) na *Mgomba Changaraweni* (Ken Walibora), wahusika wa kiume ni wengi kuliko wahusika wa kike. Wahusika wakuu katika kazi hizi mbili ni wavulana. *Mwanasesere wa Mosi* (Demere Kitunga) na *Alitoroka Kwao* (Angelina Mdari) zina wahusika wengi wa kike kuliko wa kiume. Aidha wahusika wakuu katika kazi hizi mbili ni wa kike. Matokeo haya

yanaonyesha kwamba ukosefu wa uwakilishi sawa wa idadi ya jinsia zote kunaweza kuchangia uendelezaji wa taswira dumifu za uana miongoni mwa wasomaji wa fasihi hii. Hali hii inatokana na sababu kwamba wasomaji hujitambulisha na kujinasibisha na wahusika wa jinsia zao. Kwa hivyo, *pana haja ya waandishi wa fasihi ya watoto kutunga* kazi zenye uwakilishi sawa wa wahusika wa kike na kiume.

Hatimaye, mikabala ya ufeministi wa kiharakati na uana iliyoongoza utafiti huu imekuwa muhimu ila tuligundua kwamba sababu inaafiki zaidi jamii za mataifa ya Kimagharibi kuliko jamii za mataifa ya Kiafrika. Kwa hivyo, kutokana na tahakiki mbalimbali zinazozidi kuongezeka kuhusu utafiti wa maswala ya uana, ni wazi kwamba ipo haja ya kuziendea tamaduni zetu na kuzitafakari ili zitupe suluhisho kuhusu nadharia ifaayo au zifaazo kushughulikia fasihi za Kiafrika. Hali hii inatokana na sababu kwamba, dhana za 'uana' na 'jinsia' zinavyoeleweka na nchi za Kimagharibi ni tofauti na jinsi hali ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika. Hii ni kwa sababu, baadhi ya tamaduni zetu hazizingatii sana kigezo cha maumbile (jinsia) kuainisha dhana 'mwanamke' kama zifanyavyo tamaduni nyingi za Kimagharibi. Chambilecho Ogundipe-Leslie (1998), dhana ya 'mwanamke' katika muktadha wa Kiafrika ina maana pana zaidi kuliko ule ufinyu wa Kimagharibi wa kuyatazama maumbile yake.

### 5.3 Kuhusu Nadharia Tete

Nadharia tete tatu zilizoongoza utafiti huu ni: Mosi, taswira dumifu za uana zinadhihirika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Pili, wahusika katika fasihi ya Kiswahili ya watoto husawiriwa kwa njia sawa bila kubaguliwa kwa misingi ya jinsia yao. Mwisho, waandishi

wa kazi za fasihi ya Kiswahili ya watoto huwakilisha idadi sawa ya wahusika wa kike na kiume katika kazi hizo. Kupitia kwa utafiti huu, nadharia tete ya kwanza imethibitishwa kuwa kweli. Lakini nadharia tete ya pili na ya tatu zimethibitishwa kuwa si kweli.

## 5.4 Matatizo

Katika kufanya utafiti huu, tulikumbana na matatizo ya hapa na pale ingawa hayakutuzuia kwa vyovyote kuikamilisha kazi hii. Tutazungumzia matatizo makuu pekee. Kile ambacho labda matatizo hayo yalichangia ni kuathiri ubora wa matokeo. Tatizo la kwanza ni muda mfupi uliotengewa utafiti huu. Miezi mitatu kwa hakika ni muda mfupi sana katika kufanya uchunguzi wa kiwango hiki.

Pili, tulikumbana na tatizo la ukosefu wa vitabu na maandishi mengine ya rejea kuhusu fasihi ya watoto kwa jumla na hasa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Maandishi tuliyopata ama ni kuhusu fasihi ya watoto ya mataifa ya Kimagharibi au vitabu na tahakiki kutoka sehemu hizo ambavyo vilichapishwa miongo kadha iliyopita. Hali hii inaonyesha mambo mawili. Kwanza, kwamba utafiti katika utanzu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto umepuuzwa na pili, kwamba hakuna juhudi za kimaksudi zinazofanywa kuhakiki kazi za utanzu huu. Tunaamini kwamba utafiti huu utakuwa msingi maridhawa kwa watafiti wa baadaye watakaojisosa katika uwanja huu ili kubatilisha hali ilivyo hivi sasa.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Kiini cha utafiti huu kilikuwa kwenye taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Upeo wetu umechunguza fasihi ya watoto iliyochapishwa katika kipindi cha

baada ya ukoloni hususan kati ya miaka 2001 – 2006. Kuna vipindi vya kabla ya ukoloni na wakati wa ukoloni. Hili ni eneo ambalo watafiti wa baadaye wanaweza kulitafitia hasa katika msingi wa taswira dumifu za uana.

Aidha, utafiti huu umejikita kwenye matini za kimaandishi za kifasihi. Mojawapo ya sifa kuu za fasihi ya watoto ni kwamba huwa na matini za maandishi na matini za michoro au picha zinazochangia sana katika uelewekaji wa hadithi miongoni mwa watoto. Watafiti wa baadaye pia wanaweza kuchunguza vipengele vya taswira dumifu za uana kwenye fasihi ya Kiswahili ya watoto na uwakilishi wa idadi sawa za wahusika wa kike na kiume kwenye matini ya michoro au picha.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. H. (1979) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry.* Nairobi: K.L.B.

Allport, G.W. (1954) *The Nature of Prejudice*. Garden City, NY: Doubleday.

Beauvoir, S. (1970) *The second Sex*. New York: Alfred Inc.

Cameroon, D. (1985) *Feminism and Linguistic Theory*. London: McMillan.

Chacha, N.C. (1986), 'Mazingira ya Mwanamke Katika Fasihi ya Kiswahili: Rosa Mistika wa E. Kezilahabi', In Mwamko, Na. 3.

Chakava, H. (1996) *Publishing in Africa: One Man's Perspective.* Nairobi. E.A.E.P & Religion Publishing Network. Nairobi

Chapleau, S. (2004) *New Voices in Children's Literature Criticism*. Lichfield: Pied Piper Publishing.

Chesaina, C. (1987) 'Women in African Drama Representation and Role', PhD Thesis, School of English, University of Leeds (Unpublished)

........... (1991) *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi: Heinemann.

............ (1994) Images of Women in African Oral Literature: A case Study of Kalenjin and Maasai Oral Narratives". Nairobi. N.U.P.

CLARION (2004) *An Introduction to Gender, Law and Society in Kenya*. Nairobi

Fisher – Thompson, D (1993) 'Adult Toy Purchases for Children: Factors Affecting sex-typed Toy Selection' In Journal of Applied Developmental Psychology, 14, Pp.385 – 406.

Forster, E.M. (1927) *Aspects of The Novel*. London: Penguin Books

Fox, M. (1993) 'Men Who Weep, Boys Who Dance: The Gender Agenda Between the Lines in Children's Literature' In *Language Arts* pp. 84-88.

Gachukia, E. & Kichamu Akivaga (ed) (1978) *Teaching of African Literature in Schools*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Gooden, A.M & Mark A.G. (2001) 'Gender Representation in Notable Children's Picture Books: 1995 – 1999' In Sex Roles: A journal of Research.

Harnak, I. (2003) 'Safari ya Prospa: A Novel for Children' In *Kiswahili Vol* 66, Y.M Kihore (ed). Dar es Salaam: TUKI.

Huck, C. (2001) *Children's Literature in Elementary School*. New York: McGraw-Hill.

Hunt, P. (1991) *Criticism, Theory And Children's literature*. Oxford: Blackwell.

Hurlock, E.B. (1978) *Child Development*. Auckland: McGraw-Hill Book Company

Imbosa, R. (1990) "Jazanda Katika Ushairi wa Muyaka", M.A. Thesis, Kenyatta University (Unpublished)

Indangasi, H [eds.] (2006) Preface, *The Nairobi Journal of Literature*: Children's Literature in Kenya. No 4. March 2006. Nairobi: UoN. Pp.iv.

K.I.E. (2007) *Approved List of Primary Schools Text Books & Other Instructional Materials*. Nairobi: Ministry of Education.

Kabira, W. M. & Masheti, M. (1995) *ABC of Gender Analysis*. Nairobi: FAWE. Kabira,

Kabira, W. (1994) Gender and Politics of Control: An Overview of Images of Women in Gikuyu Oral Narratives" In *Understanding Oral Literature*. Nairobi. N.U.P.

Kezilahabi, E (1971) *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kiango, D (1992) 'Taswira za Mwanamke Katika Tamthilia za Kenya Zilizochapishwa', Katika *Baragumu*, Juzuu 1 Na 1&2 Chuo Kikuu cha Maseno.

Kimutai, R. (2004) *Ndoto ya Riziki*. Nairobi: Oxford University Press.

King'ei, K. (2002) 'Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti kutoka Kenya' in Inyani Simala K. (ed) *Utafiti katika Kiswahili.* Eldoret: Moi University Press.

Kitetu, C. (2001) 'Gendered Discourses in the Classroom – Differences or Discrimination: A cultural Interpretation", In *Egerton Journal Vol. 4 No. 1,* Egerton University.

Kitunga, D. (2002) *Mwanasesere wa Mosi.* Nairobi: Focus Publishers.

Kobia, J.M. (2004) 'Taswira za Mwamake katika Njuno (Methali) za Kimeru', Tasnifu ya M.Phil. Chuo Kikuu cha Moi (Unpublished)

Lesnic-Oberstein, K. (1996) 'Defining Children's Literature and Childhood' Hunt, Peter (Ed.) *International Companion Encyclopedia of Children's literature.* London: Routledge, pp. 17-31

Lughano, R. (1989), 'Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi', M.A. Thesis, Univeristy of Nairobi (Unpublished)

Lukens, J.R., (1999) *A critical Handbook of Children's Literature.* Ohio: Addison-Wesley Educational Publishers Inc.

Matlin, M.W. (1998) 'Bimbos and Rambos: The Cognitive Basis of Distinguished Gender Stereotypes' *In Eye on Psi Chi* (Vol.3, No.2, pp13-14. New York: Chattanooga, TN.

Matundura, B. (2001) *Mkasa wa Shujaa Liyongo.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

............ (2003) 'Watoto wa Kike wangali Wabaguliwa katika Elimu' In *Taifa Leo*, May 5,2003, p 10. Nairobi: Nation Media Group.

............ (2005) *Mwepesi wa Kusahau.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

………… (2007a) *Masagisa na Zimwi Mbilikimo*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

………… (2007b) *Maadui wa Maria*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

………… (2007c) *Fahali mtoa Siri*. Nairobi: Focus Publishers.

Marjorie, R.H., (2000) *A Celebration of Literature and Response: Chilren,Books, and Teachers in K-8 Classrooms*. New Jersey: Prentice Hall Inc.

Mbughuni, P. (1982) 'The Image of Women in Kiswahili Prose Fiction', Katika *Kiswahili* Toleo la 49/1. Dar es Salaam: TUKI.

Mdari, A. (2001) *Alitoroka Kwao*. Nairobi: Focus Books.

Millet, K. (1977) *Sexual Politics*. London: Virago.

Mitchell, J. & Oakley, A. (1986) *What is Feminism*. Oxford: Basil &Blackwell.

Mohamed, M. (2002) 'Tools of Gender Analysis in Kiswahili' In Inyani, Simala K. (ed.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press, pp 85-88.

Moi, T. (1985) *Sexual/Textual Politics*. London: Routledge.

Momanyi, C. (1998) 'Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama anavyobainika Katika Ushairi wa Kiswahili', Tasnifu ya PhD, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Unpublished)

……….. (2001) 'Usawiri wa Wahusika wa kike katika Fasihi ya Kiswahili Baada ya 2000: Kuyumbisha Uhalisi', in Makala ya Kongomano la Kimataifa; *KISWAHILI 2000* proceedings, J.S. Mdee & H.J.M. Mwansoko (eds). Dar es Salaam: TUKI.

………… (2002) 'Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili' in Inyani Simala K. (Ed.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press, pp 61-69.

............ (2003) 'Kushughulikiwa kwa Mtoto wa Kike' In *Taifa Leo*, September, pp 8. Nairobi, Nation Media Group.

Momanyi, C (2005) *Siku ya Wajinga*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Morgan, J.A (?  ) 'Gender and Cultural Analysis: Marking The Territory', In *http://www.home.earthlink.net/-nomo1521/id6.html*

Muindi, A. (1990) 'Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Riwaya za S.A. Mohamed", M.A. Thesis, Kenyatta University (Unpublished)

Mule, K. (1991) "Swala la Mwanamke Katika Tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa kike katika Njia Panda", M.A. Thesis, Kenyatta Univeristy (Unpublished)

Muthubi, F.M. (2005) 'Mikakati na Mbinu za Usilimishwaji Katika Fasihi ya Watoto' M.A.Thesis, Kenyatta University, (Unpublished)

Mwangi, E. (2002) 'Artistic Choices and Gender Placement In The Writings of Ngugi wa Thiong'o, PhD Thesis, UoN (Unpublished)

Mwanzi, H.O.A. (1982) 'Children's Literature in Kenya: An Analysis of Children's Prose Fiction', M.A Thesis, UoN (Unpublished)

............ (2006) 'Children's Literature: The Concept of Socializing the Young," In *The Nairobi Journal of Literature* No 4. pp 49.

Mwita, M.B (2002) 'A quest for Understanding Kiswahili Research and Gender Issues' In Inyani Simala K. (ed.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Njogu, K & Rocha, C. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkata, D (2001) ' Continuity and Change in Storytelling: Children's Stories in Uganda's

Past and Present," In *http://www.children.org.za/acl/artnkatha.html.*

Oakley, A (1981) *Subject Women*. Oxford: Martin Robertson.

O'Keefe, E., & Hyde, J.S. (1983). 'The Development of Occupational gender-role Stereotypes: The Effects of Gender stability and Age', In Sex Roles: In *http:/www.findarticles.com/p/articles/mi_m2294/is_1112_49/ai_111635870*

Okere, I.O & Keraro, F.N (2002) 'Influences on Childhood Science Education: The Kenya Experience' In *Egerton Journal* Vol. 4 No 1. Nakuru: Egerton University.

Odaga, A. (1985) *Literature for Children and Young People in Kenya.* Nairobi: Kenya Literature Bureau. PhD Thesis, School of English, University of Leeds (Unpublished)

Odhoji, M.O.B (1997) 'Traditional Bases of Sex Differentiation In Power Relations & Control of Resources: A study of Oral Folktales of Kanyango Clan of Masumbi, Among the Luo' In Wanjiku et al (ed) *Contesting Social Death: Essays on Gender & Culture*. Nairobi: KOLA.

Ogundipe-Leslie (1998) 'Conceptualizing Gender in Africa', makala katika Jarida la AWLI, Jan. 31- Feb. 14,Entebbe, Uganda

Ostrgaad, L. (1992) *Gender and Development*. London: Routlege

Oyeronke Oyewumi (1977) *The Invention of Women: Making of an African Sense of Western Gender Discourses*. Minneapolis. University of Minnesota.

Palmer, P. (1989) *Contemporary Women's Fiction: Narrative Practice and Feminist Theory*. New York: Harvester Wheatsheaf.

Signorella, M.L., Bigler, R.S., & Liben, L. S. (1993) 'Developmental differences in

Children's gender Schemata about Others: A Meta analytic Review' In Developmental Review, 13 pp 140-183.

Simala, I (1994) 'Sexist Overtones in Kiswahili Female Metaphors: A critical Analysis', A research Project. OSSREA

Turner, P.J., Gervai, J., & Hinde, R.A. (1993). 'Gender-typing in Young Children: Preferences, Behavior, and Cultural Differences', In British Journal of Developmental Psychology, 11', pp 323-242.

Tuttle, L. (1986) *Encyclopedia of Feminism*. London: Longman.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

……… (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.*Nairobi. Focus Books.

……… (2006) *Msichana Mlemavu wa Ndugu Zake.* Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wafula, J (2004) 'Gender Relations in Ben Okri's Trilogy: The Famished Road, Songs of Enchantment & Infinite Riches' M.A. Thesis, UoN (Unpublished)

Waita, N (1997) 'Gender Conflict And Oral Art forms: An Analysis of the Patriachal/Matriachal Conflict in Inheritance and Resource Control Among the and Gichugu of Kirinyaga District' In Wanjiku et al (ed) *Contesting Social Death: Essays on Gender & Culture*. Nairobi: KOLA.